Moyo wa Jambo

Wito wa kumfuata Yesu

Nguvu za kufufuka

Kanisa ambalo Yesu anajenga

Saba MOJA

Kanisa la kibiblia la nyumbani

Kanisa linalokutana nyumbani

Kanisa la siku ya tatu

Kurejeshwa kwa vitu vyote

Mwanaume Mtoto kampuni

Asili ya watu Wanaoshinda

Kampuni ya Kitume

Paul Galligan

Revival Ministries Australia

Yaliyomo

1. **Wito wa kumfuata Yesu**
2. **Kutembea katika nguvu za kufufuka**
3. **Kanisa ambalo Yesu analijenga**
4. **Kuna moja ... wale saba Moja**
5. **Kanisa la kibiblia la nyumbani**
6. **Kanisa linalokutana nyumbani**
7. **Kanisa la siku ya tatu**
8. **Kurejeshwa kwa mambo yote**
9. **Kikundi cha mwana mume**
10. **Asiri ya watu wanaoshinda**
11. **Kikundi cha kiutume**

UTANGULIZI

Katika siku hizi Roho wa Yesu anatuita tusimame na kutafakari jia zetu. Je tunamfuata Yesu hakika au tunafanya vitu ambazo tunafikiria ziko sawa lakini haziambatani na Maandiko?

Katika **Luka 6:46** Yesu anasema "***Na ni kwanini mnaniita Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?"*** Kisha anaendelea kuongea juu ya watu wawili waliojenga nyumba; mmoja mwelevu na mwingine mjinga. Yule mwelevu alisikia yale Yesu alisema na akatii. Akayatenda maagizo ya Yesu' maneno na amri na nyumba ikasimama. Yule mjinga aliyasikia aliyoyanena Yesu lakini hakuunganisha kusikia kwake na imani ambayo ingeelekeza kwa kutii. Nyumba ya mwenye hekima ikasimama wima; nyumba ya mjinga ikaanguka.

Yesu anatuita leo kupitia neno alilolinena zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Anatuita "kuachana na yote" na kuwa wanafunzi wake; 'kuhesabu yote hasara' ili 'tumjue Yeye' na kutafakari kama "*Lulu ya thamani kubwa*" na maenzi kuwa tayari kuyaacha yote ili kupata thamani hiyo.

Anatuita tutafakari njia zetu! Tukijipata kwamba tumekuwa tukijenga juu ya mchanga katika maisha yetu binafsi na tukijipata kuwa tumekuwa tukilijenga kanisa la Yesu kwa njia yetu, twahitaji kutafakari njia zetu. Twapaswa "***Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza"*** **(Ufu 2:5).**

Yesu anatuita turejelee 'kiini cha mambo' na tuanze kujenga maisha yetu sisi wenyewe na Kanisa lake kwa njia Yake, kulingana na mwelekeo ambao ametupa katika neno lake.

Ni wakati wa 'kuhesabu gharama' na "***Basi utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake" Mathayo (6:33)*** na nifikie "***Mende ya thawabu ya mwito mkuu katika Kriso Yesu"*** **(Wafilipi 3:14)**

Nicholas Jackson, 2007

WITO WA KUMFUATA YESU

Yesu aliwaita Petro na Andrea walipokuwa wakirusha nyavu zao baharini. Akawaambia **"*Nifuateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu … mara wakaziacha nyavu zao wakamfuata".*** Vivyo hivyo Yakobo na Yohana waliitikia mara moja na wakamfuata Yesu **Mathayo 4:18-20.** Twafahamu kutoka kitabu cha Yohana kwamba mwanzo Yesu alikuwa amekutana na Andrea, Petro, na Yohana katika kikundi cha Yohana mbatizaji. Kutokana na hayo tunaweza kusema vijana hawa, Filipo na Nathanieli, walikuwa wakitazamia "***tumaini la Israeli".*** Wote walikuwa wametoka katika kijiji kimoja cha uvuvi, Bethisaida, na walijihusisha na biashara ya uvuvi, na vile vile walihusika na ufifio mkubwa uliokuwa ukifanyika katika huduma ya Yohana.

Inafurahisha kutafakari **"Ni nini ilikuwa kwa mioyo ya vijana hao"**?' Hatima yao ilikuwa imewekwa na Mungu waitwe na wachaguliwe kuwa wanafunzi wa Bwana Yesu Kristo.

- **Hatima yetu iliyowekwa na Mungu ni kuitwa na kuchaguliwa kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo**
- **Lengo la sisi kuwa wanafunzi ni kuwa na uweza kuwatuma wanafunzi walio andaliwa kwa kazi ya mavuno**
- **Bwana anatupa changamoto kutazama tena na kuirejelea mafunzo ya kimsingi ya huduma ili kuwainua wafanyi kazi kwa mavuno.**

Yesu anayewafanya wanafunzi

Yesu alianza kuwaita watu wamfuate na wawe wanafunzi Wake baada ya kurudi kutoka majaribio ya nyika. **Mathayo 4, na Luka 4** inatuambia kwamba Yesu aliongozwa na Roho katika nyika ili kujaribiwa na ibilisi. Akiisha **Kumshinda** ibilisi na majaribio, Yesu sasa alikuwa amehitimu kikamilifu kuanzisha huduma yake na sehemu yake ya muhimu ilikuwa ni kuwafanya wanafunzi. Kisha akawaandaa na kuwatayarisha baadhi ya wanafunzi hao wawe viongozi wa huduma katika kanisa lake.

1 Yohana 2:13-14 inatuambia ya kuwa "**vijana"** ni wale ambao "***wamemshinda yule muovu";*** Yakwamba vijana ni wale ***"walio na nguvu na neno la Mungu linakaa ndani yao***". Yesu amekuwa mkamilifu, jaribio la mwisho ikiwa ni ushindi dhidi ya ibilisi.

Mwanafunzi yuko tayari kuanza huduma wakati wamefika kiwango cha ushindi juu ya majaribu na Juu ya ibilisi. Nikutokana na ushindi huu tunawahudumia wengine.

Wakati mwingine kanisani mtu anaonekana akiwa na karama na wanahimizwa kuhudumu. Hata hivyo mara mtu huyu hajatayarishwa katika neno au hajaandaliwa katika huduma na hivyo huduma inayopatianwa haileti mazao ya ufalme.

Ninani alimfundisha Yesu?

Ni nini kilitendeka katika maisha ya Yesu katika kumtayarisha? Yesu akiwa Mwana wa Mungu alikuwa mtu spesheli. Hata hivyo, katika kufanyika mwanadamu Yesu alichukua kikamilifu hali yetu ya uutu. Wakati wazazi wake walimpata kwa hekalu akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, alimwambia mama yake "***Hamkujua yakuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba Yangu" Luka 2:49.*** Baada ya hayo Yesu "***akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, Naye alikuwa akiwatii…naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo akimpendeza Mungu***

na wanadamu aya 51-52. Maandiko mengine tuliyo nayo ya Yesu kabla ya ubatizo Wake ni katika **Luka 4:16,** inayo tuambia ilikuwa ni desturi ya Yesu kwenda kwa Sinagogi.

Kulikuwa na miaka kumi na minane ya Yesu kutayarishwa kwa mtu Yesu ili aichukue huduma kama Masihi.

Kwa miaka hii kumi na minane:

- Yesu **alitembea katika utiifu –** alikuwa **anawatii wazazi wake.**
- Yesu **alitembea katika neema** – kutegemea Mungu.
- Yesu **aliongezeka katika kimo**, ikiongea habari ya maisha yake yaliyonyooka.
- Yesu **alijifundisha uvumilivu**, kungonjea wakati ufike atakapojua kikamilifu mapenzi ya Baba.

Alikuwa tayari na kukamilika katika umri wa miaka therathini kuingia kwa huduma kama Masihi na kisha Mwokozi/Mkombozi. Tunaweza sema kwamba **Moja kwa moja Yesu alifundishwa na Baba yake kupitia Roho**, hata kama vile Yohana mbatizaji alifundishwa na kutayarishwa na Mungu mwenyewe.

Yesu kama Mwana anaanza huduma yake

Katika **Mathayo 3** Yesu alikuja kwa Yohana ili abatizwe. Alikuwa anatimiza "***haki yote***" **aya 15.** Ilikuwa ni katika ubatizo wake ambapo Mungu alimpaka na Roho Mtakatifu na akatangaza uwana wake. Yesu alikuwa na umri wa miaka therathini. Huu ulikuwa ni wakati wa mwana mume kukomaa, mwana aliyekomaa ambaye anaweza kuupokea urithi wa Baba. Kisha Yesu akaaongozwa katika nyika na baada ya kufunga siku arobaine na kumenyana na shetani "***wakaja Malaika wakamtumikia"*** **Mathayo 4:11.** Kisha Yesu akaanza huduma yake. Akaanza kuhubiri "***tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia"*** **(aya 17).**

Mwanzo wa huduma ya Yesu ilikuwa ni kuhubiri ufalme wa Mbinguni. Ni wachache wetu katika kuja kwa Kristo na kisha kuanza huduma, wanaelewa ya kuwa ujumbe ni **injili ya ufalme wa Mungu au injili ya Yesu aliye Masihi.** Kwa sababu hii mambo mengi yanayo semwa na kutendwa katika huduma yanakosa uhakika wa kuhubiri ufalme wa Mungu na kuwaleta watu katika ufalme kupitia kuzaliwa upya, (**Yohana 3:3-6).** Matokeo ni kwamba kanisa ni idara kubwa isiokuwa na nguvu katika jamii na sio "**Ubalozi wa ufalme wa Mungu katika kila mji na jiji kote kote ulimwenguni.**

Wanafunzi wa kwanza

Tayari tumesema kwamba wanafunzi sita walikuja kutoka kwa kijiji kimoja na watano wao walikuwa wamekutana na Yesu walipokuwa katika kikundi cha Yohana mbatizaji. Vijana hawa wakiisha kulelewa kama Wayahudi waaminifu wakiwa wanaendelesha dini za baba zao, **walikuwa wakitafuta kitu kingine zaidi** na walikuwa na sikio la kusikia vile Roho alikuwa anafanya, na kusema katika kizazi chao. Wangali wameajiriwa na baba zao katika biashara ya uvuvi walikuwa na wakati wa kuwa sehemu ya ufufuo iliyokuwa ikikamata taifa wakati huo. Kwa sababu ya mioyo yao ya jaa na kiu kwa 'zaidi'**waliweza kumtambua Yesu walipojulishwa yeye.** Kwa hivyo walikuwa **na uwezo wa kuitikia mwito wa kufanyika wanafunzi wake mara moja.** Ni wangapi wetu ambao wamekuwa wakitamani hata sasa kuitikia mara moja na kwa moyo wazi kwa mwito wa kuwa wanafunzi kwa Yesu Kristo?

Hawa watu waliviacha vyote ili wamfuate Yesu

- Waliacha **familia** zao;
- Waliacha **kazi** zao na kwa hivyo **mapato;**
- Pengine waliacha **urithi** wao katika biashara ya jamii;
- Waliacha **nyumba** na kwa Petro twajua hiyo ilikuwa kuacha mkewe, akiwa hayupo nyumbani mara nyingi na akija nyumbani anakuja na wengine kumi na wawili wakitafuta chakula!

Wengi kwa maisha yetu tumekuja katika uhusiano wetu na Yesu kupitia neno na Roho. Wengi wamekuwa na moyo wa kile Mungu anatenda na kwa hivyo kumekuwa na miondoko ya nguvu na ufufuo; makanisa mapya yamepandwa; shule za Biblia zimefunguliwa. Katika Australia baadhi ya makanisa makubwa ya kipentekote yalio faulu yanajulikana kote katika taifa na jee kati ya miaka ni wangapi wamefanyika wanafunzi wa Yesu Kristo?

Ni wangapi wameitikia mwito wa Yesu na 'kuviacha vyote' kumfuata yeye, kuwa wanafunzi na kutumwa kama wafanyi kazi katika mavuno?

Ni makanisa mangapi na vyuo vya biblia ambao wanahubiri injili ya ufalme wa Mungu na kufundisha mambo kuhusu jina la Yesu?

Ni huduma ngapi, makanisa na shule ambazo zinafundisha "***wahuduma wa upatanisho"*** ambao wanaenda katika ulimwengu kama **Mabalozi wa ufalme wa Mungu**, wakitumia mamlaka yake kama mabalozi?

Kuitikia kwetu katika mwito wa kumfuata Yesu

- Tunawaita **waamini wapya kuwa wanafunzi**
- Tukiwapa nidhamu ya kujitoa katika **kusoma maandiko, kujifundisha** na **kuomba.**
- Kuwasaidia wanafunzi kupokea, kutambua na kuitikia '**neno la Mungu lililohuishwa'**
- Kuwaelekeza wanafunzi katika **kushuhudia imani yao** mara kwa mara, wakitumainia Mungu kwa fulsa na nguvu za kushuhudia.
- Kufanya **vikundi vya uelekezi** na uhusiano wa kibinafsi na wale ambao wako tayari kwa huduma
- **Kutambua hitaji na kuwatayarisha watu katika kazi ya huduma**
- Kuwa na wakati wa kufanya mazoezi katika maeneo yafuatayo ya huduma:
  a) Jinsi ya kumuelekeza mtu kwa Kristo
  b) Kubatiza waamini kwa maji mengi
  c) Jinsi ya kuhudumu ubatizo wa Roho Mtakatifu
  d) Maelezo katika kufanya kazi katika karama za Roho Mtakatifu, **1 Wak.12:4-11**
  e) Jinsi ya kuabudu-kujifundisha kutiririka katika upako wa Roho
  f) Zoezi na kujihusisha katika maombi na uombezi
  g) Jinsi ya kuhudumu uponyaji na ukombozi
  h) Jinsi ya kujihusisha kuwafikia walio nje na uinjilisti.

Yote tuyatendayo yanastahili yawe **katika mazingira ya ufalme wa Mungu,** sio katika mazingira ya mambo tuliorithi ya mfano wa kanisa. Kanisa ni mwili sio idara! Kanisa halistahili kujiletea uhai wake- miudo yake ya kiidara, serekali na mengineo kado na ufalme. **Nguvu zote na mamlaka yote yana Yesu Kristo.** Hapatiani nguvu hizo na mamlaka hayo kwa idara ya kanisa.

Anaachilia nguvu zake na mamlaka kupitia wanafunzi wake ambao wamefundishwa na kutumwa nje katika huduma.

KUTEMBEA KATIKA NGUVU ZA KUFUFUKA KWAKE

Nguvu za Kufufuka Kwake

"*Ili nimjue yeye, uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake, ili nipate kwa njia yo yote kuifikia kiyama ya wafu"* Wafilipi 3:10-11

Paulo anaandika mambo manne ambayo anatamani kwa vyo vyote – anaamini anatakikana ajue - ***Ili nipate kwa njia yeyote kuifikia kiyama ya wafu.*** Mwanzo Paulo alikuwa amesema anayahesabu yote "***kuwa hasara kwa ajiri ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu",*** Kwamba alikuwa ameenda ***"hasara ya mambo yote",*** pasina tena kuyathamini mambo yote yaliokuwa usalama na kitambulisho – mambo yalioorodheshwa **aya 5-6**

Ufunuo huu wa mambo manne ulihitaji kutembea katika nguvu za ufufuo

1) "Kumjua yeye"

Paulo anang'ang'ana "***kumjua yeye,"*** Yesu Kristo. Mtu angesema "***hakika Paulo alikuwa amemjua vyema kuliko wengi"*** Paulo alikuwa amekomaa kwa wakati huu, katika korokoro baada ya miaka mingi ya ushindi na huduma yenye mazao, na bado alitamani sana kumjua kiundani na kiushirika.

Jambo muhimu la uzima wa milele ni kumjua Mungu.Yesu kwa kumwomba Baba kwa sababu ya wanafunzi wake alisema "***Wakujue wewe, Mungu wa Pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma"*** **Yohana 17:3**

2) "Nguvu za kufufuka kwake"

Paulo alitaka kujua "***nguvu za kufufuka kwake".*** Jambo la kuelezea kuhusu Yesu Kristo na imani ya kikristo ni kufufuka kwa Yesu Kristo, ukweli wa mambo – alifufuka toka mauti baada ya siku tatu. ***"Tena kama Kristo hakufufuka, basi kuhubiri kwetu ni bure na imani yetu ni bure"*** **(1Wakorintho 15:14).** Katika **Waefeso 1:19,** Paulo anatuombea tujue ***"ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo".*** Anaendelea kusema ***"ni nguvu zile zile aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho"*** **aya 20.**

Kujua nguvu hizi twahitaji ***"roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye" aya 17,*** na twahitaji "***macho ya mioyo yenu yatiwe nuru"*** **aya 18.** Kwa njia ingine ufahamu kama huo na ujuzi wa Kristo aliye fufuka katika nguvu zake za milele na utukufu zaweza kujulikana tu katika ufunuo: Bwana akijifunua kwa wale wanaomtafuta Mungu, waliotakaswa na kutayarishwa.

Twawezaje kuja katika mahali ambapo Bwana anaweza kutupa ufunuo wa kubadirisha maisha kama huo? **Waefeso 5:26** inatupa mwangaza, "***Kristo mwenyewe analitakasa kanisa na kulisafisha kwa maji katika neno",*** na katika **1 Wathesalonike 5:23,** ni Mungu wa amani atakaye ***"watakasa kabisa",*** na katika **1 Petro 5:10,** ni Mungu wa neema yote atakaye ***"watengeneza, na kuwadhibitisha, na kuwatia nguvu"***.

Jambo ni, Mungu anafanya kazi hii ndani Yetu. "***Maana kwa toleo moja amewakamilisha hata milele hao wanaotakaswa"*** **Waebrania 10:14.** Ni kazi ya utakaso ndani yetu inayotuachilia katika nguvu za kufufuka kwake.

Asanti Yesu, kwa neema yako na amani isiyopungua kutuleta katika ukomavu, katika ujuzi na ufahamu wa uweza wa nguvu za ufufuo.

3) "Ushirika wa mateso yake"

Kunga'ngana huku ili kumjua Yesu katika nguvu zake za kufufuka yaweza kupatikana tu kwa ***"ushirika wa mateso yake"*.** Mapema katika huduma yake kama mtume katika **Mdo 14:22,** Paulo alikuwa amewahimiza waamini wapya kusema "***imetupasa kuingia katika Ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi"***. Hii ni tofauti namna gani kwa 'kuamini kwa wepesi' ya 'kuokoka ili kwenda mbinguni'; Ni tofauti namna gani kwa 'injili ya ufanisi'; nitofauti namna gani kwa 'kuepuka kwa njia ya kunyakuliwa' mawazo ya karne ya ishirini. Mateso ya Kristo yamewakilishwa kama tiketi wakati huu na maisha yajao pamoja na yeye katika wokovu. Wakati haya yote ni ya kweli, hatujawaambia wale tunaelekeza kwa Kristo, '**Karibu kwa maisha ya kusulibishwa'.**

Mwito wa Yesu katika wokovu ni mwito wa Mateso, kuyatoa maisha yako kwake na kwa wengine, mpaka kifo. Ni Paulo alisema katika **Wakolosai 1:24 "*Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake".*** Ni Yesu aliyesema, "***ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu"* Yohana 16:33.** Yesu alishinda dhiki na mateso jinsi gani katika maisha yake-kwa njia ya msalaba na pia kwa njia ya ufufuo!!

4) "Kufananishwa na kifo chake"

Kufikia maaisha ya kufufuka Paulo anatangaza ya kwamba ni lazima "***afananishwe na kifo chake"***, Kifo cha Kristo. **Warumi 8:29** yasema "***alituchagua tangu asili tufananishwe na mfano wa mwana wake".*** Hii inahusisha kifo, sio kifo cha mwili, lakini kifo cha utu: 'ile ninataka, 'ninatamani', 'ninafikiria'; kifo cha ngome na mafikara, na vifungo tulizojiletea kwa sababu ya kiburi na upinzani ndani ya nafsi zetu kwa maisha ya Kristo ndani yetu.

Kufananishwa na mauti yake yaja kwa kutambua nguvu za Mungu zinazo fanya kazi ndani yetu kutufunulia na kufanya zijulikane kupitia sisi nguvu za kufufuka kwake. Twapaswa "***Siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu. Kwa maana sisi tulio hai, siku zote twatolewa tufe kwa ajili ya Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu ipatikanayo na mauti. Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu"* 2Wakorintho 4:10-12.** Tunapokuja "***kujua, naam tukaendelea kumjua YAHWEH"* (Hosea 6:3)** uhakika wa mauti ya Yesu ndani Yetu utadhihirishwa.

Fundisho la msingi

Mafundisho ya "***kufufuka kutoka kwa wafu***" ni msingi wa tano ulioorodheshwa katika **Waebrania 6:1-2.** Kuna misingi sita ambayo ni lazima iwekwe kabla ya kanisa lienende katika ukomavu. Mungu "***hatajalia"*** kueneda katika ukomavu kabla misingi haijawekwa, (**aya 3).** Kanisa lina baadhi ya ufahamu wa misingi ya kwanza nne: **Kuzitubia kazi zisizo na uhai na wakuwa na imani kwa Mungu –** misingi ya kwanza miwili imeunganishwa na hakika ni ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili, kuja kwa Mungu kikamilifu kwa mwaamini mpya, kwa mfano kuokoka; **mafundisho ya mabatizo** na **kuwekewa mikono** pia zimewekwa pamoja – Mtume Petro anasema katika **Mdo 2:38 *"… mkabatizwe… nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu".* Katika Mdo 8:12-17** walioamini kupitia Philipo walibatizwa na kwa kupitia kuwekewa mikono ya mitume walipokea Roho Mtakatifu. Vile vile Katika **Mdo 19:4-6** wanafunzi wa Yohana walipokea ubatizo wa wakristo na kisha Paulo akawawekea mikono wakapokea Roho Mtakatifu.

Fundisho la kufufuliwa kwa wafu

Hata hivyo tunapokuja kwa msingi wa tano na wa sita kwa jumla kunakosekana uhakika wa **kufufuliwa kwa wafu** na **hukumu ya milele** kanisani**.** Wakati sisi zote tunaweza kujua kitu juu ya mafundisho haya, ni ufunuo na ujuzi wa kiroho wa mafundisho haya yakifanyizwa kazi ambayo yanakosekana. Mungu anarejesha uhakika wa mafundisho haya ya kimsingi leo.

Uzima wa milele ni maisha ya kufufuka

- Ujuzi wetu wa kwanza katika kuzaliwa mara ya pili
- Ujuzi wetu wa ubatizo wa maji
- Ujuzi wetu wa kupokea nguvu za Roho Mtakatifu, zote ni dhihirisho wa nguvu za kufufuka za Yesu Kristo.

Uzima wa milele ambao tunapokea wakati tunapozaliwa mara ya pili ni maisha ambayo Yesu aliachilia kupitia nguvu za kufufuka kwake. **Katika Yohana 20:22** Yesu alikuja kwa wanafunzi wake na mwili wake uliofufuka, ***"Akavuvia, akawambia, pokeeni Roho Mtakatifu."*** kwa maana Yesu alikuwa ameenda msalabani *na* akakabiliana na dhambi ya mwanadamu, sasa alikuwa anaweza kupatiana Roho kwa wale waliomwamini.

Kwa mara ya kwanza tangu kuanguka kwa Adamu, wanadamu walipata uweza wa kupokea Roho wa Mungu katika maisha yao. **Yohana 3:16** yasema ya kwamba tunapomwamini Yesu tunapokea uzima wa milele. Uzima huu wa milele, ni katika kushiriki maisha ya ufufuo ambayo Yesu anaachilia kwa kufanyika mwanadamu, kifo cha kujitolea (kama upatanisho wa dhambi zetu) na kushinda kifo cha mwanadamu – matokeo ya dhambi - kwa kufufuka tena.

Katika **Yohana 11:25-26** Yesu alitangaza "***Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele."*** Katika jambo hili Yesu alikuwa anamsaidia Martha yakuwa nduguye angefufuliwa kutoka kwa kifo cha kimwili, alikuwa akitazama na kutufundisha yakwamba siku inakuja ambapo uzima wa milele ungepatianwa kwa wale wanaoamini kuwa yeye ni "***ufufuo na uzima***".

Kubatizwa katika ufufuo wa Yesu kristo

Ni katika ubatizo wa wakristo katika kutumbukizwa ambapo mwaamini mpya katika Kristo anakuja kwa kikamilifu katika nguvu za ufufuo wake. Ubatizo wa wakristo una nguvu na ni wa kweli kwa sababu ya kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Yesu Kristo. Ubatizo ni kitaburisho chetu na Kristo kwanza katika kifo chake, tena katika kuzikwa kwake, tena katika kufufuka katika upya wa maisha ndani yake **(Warumi 6:3-4).** Ni kupitia ubatizo ambapo sisi "***tunaunganika naye katika mfano wa mauti yake"*** na "***kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake" aya 5*****.** Mtume Petro pia anatufundisha ya kwamba "***ubatizo unawaokoa ninyi pia siku hizi kwa kufufuka kwake Yesu Kristo" 1 Petro 3:21.*** Maisha ya kawaida ya mkristo imesimama katika msingi huu: Kwamba kupitia ubatizo tumewekwa katika '**ufufuo wa Yesu Kristo'.**

Ujumbe wa ufufuo unaleta uzima na upinzani

Ujumbe wa mitume wa kwanza katika kitabu cha **Matendo ya mitume** iliyoleta mazao mengi, lakini pia ilisababisha upinzani kuwainukia, ulikuwa ni ujumbe wa ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu. Ulikuwa ni ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu ambao ulimtangaza Yesu "***kuwa mwana wa Mungu kwa jinsi ya roho ya utakatifu" (Warumi 1:4)*****.** Ulikuwa ni ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu ulioachilia uzima wa milele kwa wale walio mwamini Yeye. Ulikuwa ni ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu na kupaa kwake mbinguni ambayo iliachilia Roho Mtakatifu kujaza watakatifu na nguvu za ufufuo.

Kwa wakati huu Mungu anarejesha mafundisho ya kimsingi ya imani ya Kikiristo kanisani mwake ili tutembee katika nguvu za ufufuo wake ili hukumu ya kweli irejeshwe kwa kanisa katika siku hizi za mwisho.

KANISA AMBALO YESU ANALIJENGA

"Nitalijenga kanisa langu" Mathayo 16:18

Misingi ya Biblia

Kanisa ni nyumba ya Mungu na imejengwa juu ya misingi ya **mitume na manabii (Waefeso2:20).** Hakuna msingi mwingine ambapo kanisa linaweza kujengwa juu yake ila kwa msingi wa mitume na manabii ambao Mungu amepatiana kanisani kupitia Kristo kwa kulijenga kanisa. Kwa miaka 1800 **Kanisa kwa jumla halijakuwa na misingi ya kibiblia.** Baada tu ya kufunga kwa kuandikwa maandiko ya Agano Jipya, kanisa lilianza kuweka ofisi za wanadamu askofu badala ya huduma ya mtume. Askofu alikuwa anawekwa aongoze kanisa la mji kinyume na mafundisho wazi ya maandiko, ambayo husema yakuwa kanisa la kila mji huchungwa (hulishwa) na kuangaliwa na wazee. Wazee hawa walikuwa wamewekwa wakfu na mitume. **Huu ndio muundo wa Biblia. (Mdo 14:23, 20:28 na Tito 1:5)**

Kurejesha misingi sawa

Katika maandiko, wazee na maaskofu ni kitu kimoja **(Mdo 20:28; 1 Timotheo 3:1-7, Titu 1:5-9).** Hapana hali katika maandiko ambapo mzee mmoja alipewa uongozi juu ya wazee wengine au juu ya kanisa la mji; lakini uzee ilikuwa ni kwa wingi. Sasa kwa mwisho wa nyakati, **Mungu anarejesha mitume na manabii** ili kanisa la mwisho lijengwe katika msingi ulio sawa. Yesu anakuja kwa kanisa lake, lililo jengwa kwa njia yake, sio kwa mikusanyiko ambayo watu wamechanganya na sasa wanajaribu kuiweka pamoja, pasina kutambua maandiko vyema na muundo uliodhihirishwa ndani.

Jiwe la pembeni

Maandiko yanasema **Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni (Efe 2:20).** Jiwe la pembeni katika mjengo linawekwa baada ya msingi kuinuliwa, katika maandiko tuna kanisa moja tu, kanisa limejengwa katika msingi usio wa kidini wa mitume na manabii ambao wamechaguliwa kanisani na Mungu mwenyewe (**1 Wakaorintho 12:28).** Kanisa ambalo limeinuka kihistoria halijajengwa juu ya msingi wa manabii na mitume na kwa hivyo tuna migawanyiko mingi ya kidini katika kanisa kwa maana watu wamefuata uongozi wa tamaduni za watu.

Kanisa la Yesu Kristo sio kuja pamoja kwa dini nyingi zilizogawanyika lakini ni kanisa ambalo limerejeshwa kulingana na maandiko.

Mara tu misingi ya kibiblia inarejeshwa na Yesu Kristo anakubaliwa na kupokelewa tena kama jiwe la pembeni, "***katika yeye njengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye nyinyi mmejengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho."*** **(Waefeso 2:21-22).** '***Hekalu takatifu'*** yaweza kuonekana kuwa ni kanisa lote la ulimwengu ambalo Mungu anainua. Hata hivyo kila mahali, kanisa la pale pale linainuliwa, ambalo limeundwa na mashirika mengi. Nikatika ushirika wa pale pale ambapo mshirika mtakatifu binafsi anapata nyumba yake ya kiroho na, **'anakamilika',** hivyo ni kutengenezwa kikamilifu kufanya kazi na kuhisi Mungu kati yao.

Ufunuo wa siri

Vitu vyote kukusanywa ndani ya Kristo

Mungu atatupa "***Roho wa ufunuo na hekima katika kumjua yeye"*** **(Waefeso 1:17).** Siri hii inafanyishwa kazi katika kuvikusanya vyote katika Kristo, vitu vilivyo mbinguni na duniani **(Waefeso 1:10).** Hii inaongea juu ya kuja kwa Kristo katika **1 Wathesalonike 4:13-18,** wakati Mungu atawaleta pamoja na Yesu wale waliokufa hao ni, waliokufa ndani ya Kristo **(aya 14).** Wakati Bwana atakaposhuka kutoka mbinguni ***"Waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza"*** **(aya 16)** ***"Kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani:*** **(aya 17).** Huku ni kukusanya yote ndani ya Kristo ili kukaribisha majira mapya ya Kristo kutawala na kutamalaki pamoja na kupitia watakatifu wake.

Imefunuliwa na Roho

Ufunuo wa siri **"Umefunuliwa mitume wake watakatifu na manabii" (Waefeso 3:5)** ili sasa "***Utajiri wake Kristo usiopimika"*** unaweza kuhubiriwa **(Waefeso 3:8),** ikielekeza *"**hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa Roho kupitia kanisa***" **(Waefeso 3:10)**. Lengo la Mungu ni kuondoa kikamilifu nguvu na mamlaka katika ulimwengu waroho na kuliweka kanisa lake pale. Kanisa hili linafahamu siri kwa sababu **siri za Kristo zisizo julikana zinahubiriwa na mitume na manabii ambao Mungu amechagua, ikiwawezesha watakatifu kufahamu na kutembea katika ufahamu wa siri.**

Ufunuo wa kanisa la kweli

Ni wakati kanisa linakuja katika ufunuo wa ufahamu wa siri ya mapenzi ya Mungu ikifanya kazi kupitia kanisa duniani kwamba utukufu wa Mungu utafunuliwa. Ufunuo huu ni ufunuo wa kanisa la kweli kama vile limefunuliwa na Roho.Roho anapatiana ufunuo kwanza kwa mitume na manabii ambao kisha kupitia ***"neema ya Mungu niliopewa"*** **Waefeso 3:2,** kuhubiri utajiri wa Kristo, ikiwezesha watakatifu wote "***na kuwaangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri hiyo"*** **(aya 9).** Kuna mengi sana ambayo watakatifu wanastahili kuingia ndani yeke; Mungu anataka kujulisha "***utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu"*** **(Waefeso 1:18).** Mpaka sasa watakatifu wengi hawajasikia mahubiri ya Kristo kwa njia ya kufunua siri.

Ufahamu wa siri ulifichwa

Siri hii ***"tangu zamani zote ilisitirika katika Mungu"*** **(Waefeso 3:9).** Wakati Mungu aliumba vitu vyote kupitia Yesu Kristo siri hii, inayoitwa ***"Hekima iliyofichwa"*** **(1Wakorintho 2:7),** ilikuwako wakati wa kuumba lakini haikujulikana wala kueleweka. Paulo anasema katika **1 Wakorintho 2:6** hekima hii haieleweki na watawala wa mapepo ya wakati huu lakini itaeleweka na watakatifu ambao wamefika kiwango cha ukomavu katika ufahamu wao katika ukristo, wakiyajua mawazo ya Kristo **(1 Wakorintho 2:16).** Katika historia yote watu katika masomo yao na katika jamii za makabila wametafuta hekima hii nje ya Kristo. Hekima hii ya ndani inaweza kujulikana kwa njia ya injili, ikifunuliwa na Roho Mtakatifu.

Kuondoa nguvu za mapepo

Kanisa linapokuja katika ufahamu wa ufunuo wa 'Kristo ni nani', na yakuwa kanisa ni ***"Mwili wake yeye avijazavyo vyote ndani ya vyote"***, kisha ufunuo huu utajulika na watawala wa mapepo kupitia kanisa (**Waefeso 3:10).** Mabadiriko makubwa yamepatikana kwa sababu Yesu alikufa msalabani. Matunda ya kifo chake na kufufuka ni kujengeka kwa mwili wake, Kanisa. Kanisa lake linapounganishwa kweli katika Kristo ambaye ni kichwa kisha hekima ya Mungu ya

namna nyingi, unaeleweka na kanisa kupitia mahubiri ya neno la kiunabii, yajaza ulimwengu waroho, ikihamisha utawala na uongozi wa nguvu za kipepo. Nguvu hizi sasa zinatawala kupitia udanganyifu na dini za uongo. Wakati kanisa litakuja kujua ufahamu wa siri, falme za mapepo zitatii kikamilifu ufalme wa Kristo. "***Zitapiga goti na kukili yakuwa Yesu Kristo ni Bwana kwa utukufu wa Baba"* (Wafilipi 2:10-11).**

Ufunuo wa siri unaachilia utukufu

- Hekima hii si ya watoto wachanga – watoto wanahitaji ***'maziwa ya neno'***
- Hekima hii si ya watoto – watoto wanahitaji ***'nyama ya neno'***
- Hekima hii ***'manna iliyofichwa'*** kwa wale wanaokomaa
- ***"Mungu aliiweka hekima hii kabla ya nyakati kwa utukufu wetu",*** na sasa Roho anatufunulia siri hii **(1 Wakorinto 2:10).**
- Hekima hii haijulikani kwa ujuzi wa mwanadamu; ni kwa ufunuo kwa roho ya mwanadamu.
- Kuhakikisha kwamba watakatifu wake wanafahamu ufunuo wa mapenzi yake, hakika Mungu ametupa ***"nia ya Kristo"* (1 Wakorintho 2:16).**

Hii inamaanisha ya kwamba wakristo ambao wamekomaa, na pia wale ambao ni vijana, wanaweza kulifahamu neno la Mungu; hakika wanaweza kuyawaza mawazo ya Mungu. Mungu daima anafanya kazi kutimiza ***"kusudi lake la milele",*** amekwisha kukamilisha kusudi lake la milele ***"katika Kristo Yesu Bwana wetu"* (Waefeso 3:11),** na sasa ni kwa jia ya kanisa ya kwamba utendaji wa kusudi la Bwana la milele utaonekana.

Ni wakati wa kufahamu siri

Kustaabisha, Mungu sasa amekabithi ufunuo wa siri hii ya kusudi lake la milele katika upumbavu wa kuhubiri.

Katika siku hizi za mwisho Mungu anapatiana tena hii neema yake kwa mitume na manabii wake ili wajulishe ufunuo wa siri hii.

Ni kwa mtume Paulo ambapo Yesu alichagua kufunua ukweli mwingi na wa ndani wa siri ya kanisa lake. Hata leo wahuduma wengi walio na vipawa wanaomaanisha wanapinga kile Mungu anachotenda. Wengi kwa kujua wanakataa kuwapokea mitume ambao Yesu anainua nyakati zetu. Wengi wanatetea idara za kikristo, isivyostahili, isivyohitajika, kinyume cha maagizo na mafundisho ya maandiko. Katika siku zake Paulo aliwaita wahubiri kama hao Judaizers. Walikuwa wakijaribu kuingiza kanisa jipya la Kikristo ndani ya idara na tabia za kiyahudi. Walimu wa kidini wa vizazi nyingi na wale wanaowasikiza, wanakosa kwa ufunuo wa siri, ambayo ni ya umuhimu mkubwa wa kutukuzwa kwa kanisa. Watu kama hao hawana maono ya kanisa ila tu kwa kile wanachokijua.

KUNA MOJA – Zile saba moja

"Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama mlivyo katika tumaini moja la wito wenu, Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja; Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote aliye juu ya yote na ndani ya yote" **Efe 4:4-6**

Kuna saba moja zilizo wakilishwa katika aya hizi na hizi saba moja zinategemewa nani msingi wa kudumu katika kuendelea kwetu kwa kutembea na Bwana katika kufunuliwa kwa kusudi lake katika mwisho wa siku hizi. Kwa mamia ya miaka mingi kilichoitwa kanisa na wale ambao ni Wakristo wamekuwa wametatanikiwa na kuwa katika kutokukubaliana na migawanyiko juu ya mitazamo mingi ya saba moja zilizo tajwa katika aya hizi.

Wakati umefika ambapo ombi la Bwana wetu katika **Yohana 17** linajibiwa na Bwana Mwenyewe anapo likomarisha kanisa kwa njia ya kuwarejesha mitume na huduma zote tano za **(Waefeso 4:11).** Karama hizi zinapatianwa kwa "***kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe"*** **Efe 4:12.** Kukamilisha na kuwajenga watakatifu hakika inamaanisha 'kuuweka mwili katika mpangilio ili kila mshiriki akatende kazi vyema na kikamilifu.' Hii itatendeka tu kama huduma tano mtume, nabii, mwinjiristi, mchungaji na mwalimu, "***Wanatenda kazi ya huduma"*** ambayo Kristo kichwa cha kanisa, ambaye analijenga kanisa lake mwenyewe, anapatia kila muhuduma kufanya.

Kuna mwili mmoja

Mwili ni kanisa na Kristo ni "***kichwa cha mwili, kanisa"*** **(Wakolosai 1:18).** Mwili wa Kristo umeudwa na viungo vingi na kila kiungo kimeunganishwa kwa mwili kupitia ubatizo (**1 Wakorintho 12:12-13).** Tumewekwa kama viungo kwa mwili na Mungu, kulingana na mapenzi yake mema **(aya 18).**

Mwili hauwezi kugawanywa. Mwili wote wapaswa kuwa mmoja "***Ukiungamanishwa na kushikanishwa"*** kwa kichwa – Kristo **(Waefeso 4:15-16).** Kama ilivyo na mwili wa kawaida, viungo hupokea uzima na vilevile kutenda kazi vyema wakati 'zimeungamanishwa na kushikamanishwa' katika mwili. Mtume Paulo alionyesha kuhusika sana na kuleta marekebisho kwa kanisa la Korintho aliposikia ya kwamba wamegawanyika kwa kuwafuata watu mbali mbali [viongozi kama Apolo na kefa na Paulo **mwenyewe (1 Wakorintho 1:10- 13)**

Kuna Roho mmoja

"***Hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu"*** **(1Wakorintho 2:12).** Roho wa Mungu ametajwa kwa maneno {majina} mengi ya kumshukuru katika maandiko. Kwanza anaonekana katika ***Mwanzo 1:2, akiitwa "Roho wa Mungu"*** na katika sura ya mwisho ya Biblia (**Ufunuo 22:17)** na bibi harusi kanisa, ***"Roho na Kanisa wanasema, joo!"***

Roho ni:

- ***Roho*** wa Baba (**Mathayo 10:20)**
- ***Roho*** wa Bwana **(Luka 4:18)**
- ***Roho*** Mtakatifu **(Luka 11:13)**
- ***'Roho'*** [mara nyingi anaitwa tu 'yule Roho']
- Yesu alisema ***"Mungu ni Roho"*** **(Yohana 14:24)**

- Yule ***"Roho wa kweli***" **(Yohana 14:17)**
- Yule ***"Roho wa uzima katika Kristo Yesu" (*****Warumi 8:2)**
- Yule **"*Roho wa Mungu*" (Warumi 8:9)**
- Yule ***"Roho wa Kristo"* (Warumi 8:9)**
- Yule "***Roho wa Yesu Kristo" (Wafilipi 1:19)***
- ***"Roho wake yeye aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu***" **(Warumi 8:11)**
- Yule ***"Roho wa kufanywa wana"*** (**Warumi 8:15)**
- Yule ***Roho wa neema*** (**Waebrania 10:29)**
- Yule Roho ni "***Roho yule yule"*** ambaye anajidhihirisha kupitia karama za Roho kuujenga mwili **(1 Wakorintho 12:7-11)**
- Ni ***"kwa Roho mmoja tumebatizwa katika mwili mmoja"*** (**1Wakorintho 12:13)**
- Tunapaswa kuishi na ***kutembea katika Roho*** (**Wagalatia 5:15)**
- Kanisa linatakiwa kuwa ***"makao ya Mungu kupitia Roho"* (Waefeso2:22)**
- ***"Sasa Bwana ni Roho na ambapo Roho wa Bwana yupo, kuna uhuru"* (2 Wakorintho 3:17)**

Kuna tumaini moja la mwito wenu

Tumaini moja ni lipi? Wito wetu ni nini? Twapaswa kuwa na uweza wa kuyajibu maswali haya mawili vyema kutoka kwa maandiko ili kwa neema "***tulishike lile ambalo kwa aJili yake nimeshikiwa na Kristo Yesu,"* (Wafilipi 3:12),** na "***kukaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu*" (aya 14).** Wito ni ***"wito mkuu".*** Tumaini ni ili tunapo "***onekana katika yeye, tusiwe na haki yetu, …. bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo"* (aya 9)**. Hakika tuna lengo la ajabu [tumaini] katika kumfuata Kristo.

Kilele cha kueleza mwito huu chapatikana katika (**Wakolosai 1:27).** Tunapokuja kujuwa utajiri wa utukufu wa siri ya neno la Mungu, hapo Kristo anadhihirishwa ndani yetu. Maandiko yanasema "***Kristo ndani yako ni tumaini la utukufu".***

Warumi 8:29-30 inatufundisha kuwa "***Mungu alituchagua tangu asili tufananishwe na mfano wa mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi".*** Hili ndilo tumaini: kufananishwa na mfano wa Mwana wake. Mpaka mwisho huu, Mungu alituita. Akiisha kutuita akatuhesabia haki na hakika amekwisha kupatiana kutukuzwa kwetu kikamilifu ndani ya Kristo.

Katika **Waefeso 1:17-19,** Paulo anaomba tupate kujuwa kwa njia ya ufunuo ***"tumaini la wito wake".*** Tumaini hili ni "***tumaini lenye Baraka"*** kuona yakuwa tunatarajia ***"ufunuo wa utukufu wa Kristo, Mungu mkuu na mwokozi wetu"* Tito 2:13.** Tumaini hili ni nanga ya roho ***zetu "Iingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia"*** daima ikituita **(Waebrania 6:19).** Zote tuna tumaini moja na hii ndio tumeitiwa kutukuzwa ndani ya Kristo na pamoja naye.

Kuna BWANA mmoja

***"Sikiza, Ee Israeli, Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja" (*Kum 6:4).** Yesu alinukuu ilivyo katika **(Mariko 12:29).** Petro alitangaza siku ya pentekote, tena akiwazungumzia Waisraeli ***"Basi nyumba ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyu mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo"* (Mdo 2:36).** Hapana shaka yakuwa Petro alikuwa akitangaza kwa nyumba yote ya Israeli ya kwamba Yesu ni BWANA wa Agano la kale. Hii ndio

iliwachoma moyo! ***"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lipitalo kila Jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Baba"*** **(Wafilipi 2:9-11).**

Jina la Bwana ni siri kwa wengi katika Agano la Kale na kwa tafsiri ya Kingereza sana sana hawakutafsiri Jina la Mungu kama ilivyo funuliwa kwa Musa katika **Kutoka 3:14** na kisha imetumika zaidi ya mara 6500 katika Agano la Kale. Wakati neno la kingereza 'bwana' limeandikwa 'BWANA' katika Agano la Kale inazungumza habari za jina la Mungu. Tafsiri ya kingereza 'Yahweh' au 'Jehovah' [ni tafsiri ya kale lakini sio sawa] ni kweli kiasi katika Kiebrania. Katika Agano Jipya hakuna shaka yakuwa Yesu ndiye Bwana na kwamba jina lake ni Yesu.

Kuna IMANI MOJA

Imani moja yazungumzia ***"Wokovu ambao ni wetu sisi sote"*** na **Juda** anatuhimiza ***"Kushindania imani tuliyokabidhiwa watakatifu mara moja" aya 3.*** Paulo anasema alama ya kwanza ya ukomavu ni ***"Umoja wa imani"*** **(Waefeso 4:13).**

Imani ni maungamo yetu: inahusisha nia zetu kwa Biblia – kama tunaamini hakika "***Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu,"*** **(2 Timotheo 3:16).** Imani Moja ndiyo fundisho lenye mamlaka ya mitume, ambayo yalifanyika maadiko matakatifu.

"Ni mafundisho ya kiutume" ambayo kanisa lakwanza lilidumu ndani yake **(Mdo 2:42).**

Inajumuisha "***Elimu ya kwanza ya mafundisho ya Mungu"*** ambayo ni kanuni za kimsingi ya "***Kuzitubia kazi zisizo na uhai, na kwa kuwa na imani kwa Mungu, na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa kwa wafu na hukumu ya milele"*** **(Ebr5:12-6:2).**

Kanisa ulimwenguni kote linaitwa lirejelee kuimarishwa kikamilifu katika Elimu ya Msingi wa imani ili kuwapa ufahamu kamili watakatifu wote 'wokovu ambao ni wetu sisi sote', kwa maana kuna IMANI MOJA tu.

Kuna ubatizo mmoja

Yesu alipatiana utume mkuu baada ya kufufuka kwake, kitambo kabla ya kupaa kwake. **Katika Mathayo 28:18-20** na **Mariko 16:15-16,** Yesu anaamuru ubatizo kama jambo la kimsingi lenye umuhimu mwingi sana katika wokovu wa nafsi zetu. Yesu mwenyewe alikuwa ameweka mfano kwa kubatizwa ***"kutimiza haki yote"*** **(Mat 3:15).** Yesu alibatizwa katika utiifu wa Baba kulingana na neno lake.

Waumini wapya katika Yesu Kristo lazima wabatizwe kwa utiifu wa amri yake. Hili jina 'ubatizo' ni 'kutumbukiza', hii ni kuwekwa ndani ya maji. Katika maandiko maji hayakunyunyizwa bali damu ndiyo iliyonyunyizwa. Ubatizo wa maji unafuata toba na imani (**Mdo 2:38: Mariko 16:16).**

Ubatizo wa maandiko ni katika **maji, kupitia Roho, katika Kristo;** Katika kifo chake, kuzikwa na kufufuka **(1 Wakorintho 12:13 na Warumi 6:4-5).**

Kuna MUNGU MMOJA NA BABA WA WOTE, aliye juu ya vyote na kupitia vyoye, na ndani yenu nyote.

Aya hii ni ya ajabu kuonyesha kuweko kwa Mungu kila wakati, hali yake ya kuwa kila pahali! Mungu mkuu amejifunua kikamilifu juu ya Mwana wake Yesu Kristo. **Yohana 1:18** inasema ***"Hakuna mtu aliyemuona Mungu wakati wowote; Mungu Mwana pekee aliye katika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua."*** Mungu kiundani anafahamu yale yanafanyika katika maumbile yake. Yesu alisema ***"Je! Mashomolo wawili hawauzwi kwa senti moja? Wala hata***

mmoja haanguki chini asipojua Baba yenu; lakini ninyi, hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote" **(Mathayo 10:29-30).**

Yesu alimfunua Mungu kwetu kama **'Baba'.** Katika injili Yesu anamjulisha Mungu kama Baba zaidi ya mara 170 na kwingineko katika agano jipya 'ubaba' wa Mungu ameonyeshwa ikiendelea. Paulo anasema ***"Kwa hivyo nampigia Baba magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na duniani unaitwa"*** **Efe 3:14-15.**

Hata wasioamini wamefunikiwa na uwepo wa Bwana; ***"Kwa maana ndani Yeke yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu"*** **(Mdo 17:28).**

Niwakati wetu sisi sote tunaomwaamini Yesu Kristo, tukiisha kubatizwa katika mwili wake, kuwa makini na kupokea roho wa hekima na ufunuo katika ufahamu wa hizi saba MOJA ili tuwe MMOJA kama vile Yesu anatamani na ameomba.

KANISA LA KIBIBLIA LA NYUMBANI

Kwanini kanisa la nyumbani?

Kanisa la kiutume linaporejeshwa twahitaji kufundisha kutoka kwa maandiko kuhusu kanisa la nyumbani au kanisa linalo kutana nyumbani. Muundo na utendaji wa 'kanisa la pale pale hivi karibuni haikubaliki kimaandiko, ila tu tutakapoona kanisa la pale pale wakikutana kama kanisa la nyumbani katika kumbi za kukondesha; lakini hivi sivyo hali ilivyo. Hile hali ya nyumba zilizo wekwa wakfu ambazo hazitumiki kila siku kama sehemu ya kila siku ya maisha ya kiroho sio ya kimaandiko. Hatuhitaji kujenga madhabahu ya Mungu hapa ulimwenguni kwa maana kuna madhabahu moja tu iliyotajwa katika ***Ebr 9:11-12, 24.*** Katika ***Mathayo 18:20*** Yesu anasema ***"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao".*** Haya ni madhabahu, wawili au watatu wamekutana na Yesu akiwa miongoni mwao.

Kanisa la mjini

Katika maandiko mitume waliandikia **kanisa la mjini.** Katika Yerusalemu kanisa liliongozwa na mitume na wazee [ambayo ilihusisha manabii, [**Mdo 15:22, 32].** Katika Antiokia kanisa liliongozwa na manabii na walimu **(Mdo 13:1),** na kutoka **Mdo 14:23,** desturi ilikuwa ni mitume kuwaweka wakfu wazee kila mahali. Kulikuwa na kanisa la mjini pengine likiwa na uongozi wa kiutume au wazee waliowekwa wakfu ya kiutume.

Kukutana nyumbani

Katika maandiko **kanisa la mjini lilikutana katika nyumba tofauti tofauti**. Mitume walihudhulia mikutano na kufundisha mafundisho ya kiutume, (**Mdo 2:42, 20:20).** Kuendelea kwa makanisa ya pale pale yenye idadi ya mamia na maelfu ya watakatifu sio maendeleo ya kibiblia. Kanisa linalokutana nyumbani kwa kuelezea lina idadi ndogo. Hii inamaanisha ya kwamba **kila mtu aliyeokolewa moja kwa moja anahusishwa kwa maisha ya kanisa.** Kanisa la mjini kwa wakati litaongezeka kufikia mamia na maelfu ya watakatifu lakini walikutana kwa nyumba wakiwa na uongozi wa wazee wa mji.

Kanisa lilikutana wapi?

Kanisa lilikutana nyumbani

Hakuna uhakika wa kanisa moja kubwa katika Agano Jipya ila tu katika hekalu Ya Yerusalemu katika siku za kwanza za maisha ya kanisa. Jambo lisilo na ubishi katika Agano Jipya ni kwamba **walikutana nyumbani. Mdo 2:46-47** inatuambia walikutana kila siku, kutoka nyumba kwa nyumba; hitaji la kila mtu lilikutanwa nalo katika ushirika; walimega mkate pamoja, wakaimba sifa kwa Mungu na watu waliokolewa kila siku.

Kuimarisha kanisa katika kila nyumba ya rafiki.

Kanisa linapotanda kote mjini na jijini wanafunzi waliyafuata maagizo ambayo Yesu alikuwa amewapatia katika **Mathayo 10:6-15** na **Luka 10:1-12, kuimarisha kanisa katika nyumba za kirafiki.** Katika kitabu chote cha matendo ya mitume na barua za Paulo kuna matukio mengi ya kanisa kukutana katika nyumba.

Paulo anasalimia mashirika kadhaa katika Roma

Kwa mfano katika **Warumi 16:3** kulikuwa na kanisa katika nyumba ya Priska na Akila; katika **aya 10,** Paulo anasalimia watu wa nyumbani mwa Aristobulo; Katika **aya 11** anasalimia watu wa nyumbani mwa Narkiso; katika **aya 14** anasalimia ndugu walio pamoja; katika **aya 15**

anasalimia watakatifu walio na ndugu watano waliotajwa. Kuna makanisa matano ambayo yametajwa na shirika hizi ni sehemu ya Roma ambayo Paulo anaandikia.

Ujuzi katika Myanmar

Katika umoja wa Myanmar (uliojulika kama Burma) Kanisa la kwanza haliruhusiwi na mamlaka kujenga majengo yaliowekwa wakfu ya kanisa. Hii ni Baraka iliyo fichwa – kumekuwa na hasila miongoni mwa waamini katika sheria hiyo.

Kanisa linakutana kutoka nyumba kwa nyumba. Baadhi ya mikutano ya nyumba ambayo inakutana ili kupokea mtume anayetembea inaweza kufikia mia moja, lakini ni watu 20-40 wanao kutana. Katika mikutano kama hiyo kunaweza kuwa na watu wengi hata nusu yao kuja katika wokovu. Ni ya kibiblia sana.

Katika tukio moja mahali palipotengwa sana Roho Mtakatifu alikuja kama siku ya pentekote katika nyumba iliyojaa, watu sitini, watu wengi miongoni walikuwa ni wanafunzi wa shule. Wanafunzi na watu wazima walikuwa wakiongea kwa lugha (Pamoja na kingereza ambacho hakika walikuwa hawakijui), wakitabiri, wakiimba nyimbo mpya katika roho na wakiugua katika maombezi yandani. Wengine walivutwa kutoka mtaa na kuja kujionea yaliyo kuwa yakitendeka.

Kanisa la kwanza katika nyumba

Inaweza semwa yakuwa kanisa la kwanza katika Biblia lilikutana katika Bustani la Edeni, wakati wa jua kupunga katika mahali pa Adamu na Hawa. Hapo ndipo walipokuwa wakikutana na BWANA.

Yesu alisema katika **Mathayo 18: 20,** wakati wawili au watatu wanakusanyika kwa jina lake atakuwapo pale pamoja nao. Katika Yesu ushirika wetu na Mungu umerejeshwa, na ushirika huo una Mungu wakati wote tukutanapo kwa jina lake. Tumebarikiwa kufurahia ushirika wa Bwana wetu “wakati wa jua kupunga”

Ni nini kilichotendeka katika kanisa la nyumbani mwa Adamu na Hawa?

Tunakisia BWANA Mungu alifunza neno, akiweka wazi kwa Adamu na Hawa kusudi la kiungu lilikuwa nini na kuwaonya wajihadhali na ujaja wa shetani, hivyo ni, wasile kutoka kwa mti wa kufahamu mema na mabaya. Yesu alisema mkiwapokea mitume mumenipokea mimi **(Mathayo 10:40).** Yesu angali anakuja miongoni mwa watu wanaokutanika pamoja kwa jina lake.

Mtu anaweza kufikilia kwamba maisha katika nyumba ya Adamu baada ya kufukuzwa kutoka kwa shamba, ilihusisha **Adamu kuwafundisha wana wake kutembea pamoja na Mungu.** Katika hesabu ya Mwanzo 4 tunawaona Kaini na Abeli walikuwa wana uhusiano wa kibinafsi pamoja na Mungu na walikuwa wamefundishwa juu ya fundisho la ukombozi kupitia sadaka ya mwana kondoo.

Mpangilio wa Mungu kutoka Sethi mpaka kwa Nuhu inaonyesha mafundisho ya kuendelea kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika nyumba za baba zao. Kila mwana mzaliwa wa kwanza alipewa jina kiunabii na kufundishwa katika ufahamu wa kusudi la ukombozi wa Mungu. Hatimaye katika jamii ya Nuhu, mke wake na wanawe watatu na wake zao, wote walihusika katika ujenzi wa Safina ya wokovu katika kizazi hicho. **Kanisa la nyumbani, iliyohusisha jamii hizo zote nne, walifanya kazi pamoja chini ya uongozi wa kiutume wa Nuhu.** Hi ilikuwa kazi kuu walioitiwa, lakini kazi tulioitiwa ina umuhimu ule ule tunapo tengeneza Safina ya wokovu katika kizazi chetu kupitia huduma ya Biblia ya **kupanda kanisa kila mahali katika nyumba za kirafiki.**

Ibrahimu kiongozi aliyefaulu sana wa kanisa la nyumbani

"Kwa maana nimejua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya BWANA, wafanye haki na hukumu, ili kwamba BWANA naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake" Mwanzo 18:19. Mungu alimchagua Ibrahimu kwakuwa alitangulia kuona yakuwa ataiongoza nyumba yake vizuri na atahitimu kufanyika Baba wa Mataifa Mengi, akiachilia baraka ya imani kwa kila jamii **(Mwanzo 12:3).** Baraka hii ni kupitia Kristo na ni ya kila jamii.

Kimsingi kanisa linapandwa nyumbani: ni kanisa la kijamii

Kabla ya Ibrahimu kumzaa Isaka mwanawe, alikuwa na **wana wengi wa kiroho. Mwanzo 14:14** inatuambia alikuwa na watumishi 318 waliofundishwa katika nyumba yake, ambao wangeenda katika vita na yeye. Endapo watu wengi miongoni mwa hawa watu walikuwa wameoa fikiria ni nafsi ngapi zingekuwa chini ya uangalizi wa Ibrahimu. Hakika kanisa hili la nyumbani lilikuwa ni kijiji kilichotembea: mamia ya watu wakikaa katika hema, wakiangalia makundi yao. Na huu ulikuwa ni mwanzo wa huduma ya Ibrahimu.

Katika **Mwanzo 18:1-15 BWANA mwenyewe alimtembelea Ibrahimu na Sarah katika hema yao.** Hapa ndipo Ibrahimu alitabiri juu ya kuzaliwa kwa Isaka. Neno la BWANA lastahili kuachiliwa katika kanisa la nyumbani. **Wakati wawili au watatu wamekusanyika katika jina lake, 'mimi ndiye' ako pamoja nao. HALLELUJAH!** Tunapo shiriki katika imani ya Ibrahimu tunapokea Baraka.

Mungu atatutembelea katika ushirika wetu
na neno lake litakuwa la thamani na lenye nguvu

Mwana kondoo kwa kila nyumba

Tukisoma katika **kutoka 12** inatufunulia ya kwamba waisraeli wakitoka Misri, waliishi katika nyumba ambazo zilihusisha zaidi ya mtu wa jamii wa karibu. Mungu alimuagiza Musa kwamba ni lazima kila nyumba imtayarishe mwana kodoo (**kutoka 12:3).** Kama nyumba ilikuwa ndogo kumaliza kondoo yote, wangeungana na nyumba nyingine ndogo **(aya 4).** Palikuwa na kikundi kizuri cha watu kuifanya nyumba, na katika mazingira haya inaonekana palikuwa na idadi nzuri iliyopatikana. Haya ni mafundisho ya kupendeza.

> **Mungu amepatiana mwana kondoo kwa kila nyumba. Kwa kila ushirika wa watu wa Mungu ambao walikuja pamoja pana mwana kondoo. Katika nyumba ya kanisa ya agano jipya, Mungu amepatiana mwana kondoo, Mwana wake. Kila nyumba [Kanisa la nyumba] imepewa na imeruhusiwa kuumega mkate nyumbani (Mdo 2:46)**

Yesu Kristo ndiye Mwana kondoo kwa kila nyumba.

Kuna mfano mzuri wa hii katika **Mdo 10** wakati Petro alikaribishwa kwenda katika nyumba ya kornelio kushiriki habari njema za Yesu Kristo na Kornelio pamoja na jamii yake na marafiki wa karibu. **Waliokutana nyumbani walimpokea Yesu mwana kondoo wa Mungu, kupitia mahubiri ya mitume.** Kama vile Mungu alipatiana ukombozi kwa watu wake Misri kupitia Musa, nyumba kwa nyumba, hivyo sasa amepatiana wokovu kwa watu wote kupitia Yesu Kristo. Yesu amewachagua mitume na wahuduma wengine kuimarisha kanisa katika kila nyumba itakayompokea.

Maagizo ya Musa kwa kanisa la nyumba

Musa alifundisha jinsi kanisa la nyumbani linapaswa kufanya kazi kila siku (**Kum 6:4-9).** Watu wa Mungu wakimpenda Mungu kwa mioyo yao yote na nafsi zao na nguvu zao lazima wafanye kazi kama waamini siku baada ya siku.

"***Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya mimo ya nyumba yako na juu ya malango yako"*** **(Kum 6:7-9)**

Kuimarisha kanisa la nyumbani

Kanisa linaimarishwa katika nyumba ya 'kirafiki' na wahubiri [mitume, wainjilisti, wachungaji ama wanafunzi kama katika **Matendo 11]** Wakiwa wametumwa nje katika mapenzi ya Bwana. Katika **Luka 10:1-24** Yesu anatupa maagizo wazi ya kuimarisha kanisa la nyumbani katika kila mahali.

Kuenda kila mahali kabla Bwana hajakuja. Bwana aliwachagua wengine sabini; akawatuma wawili kwa wawili, kabla yeye aende, kwa kila eneo yeye angeenda. Twapaswa kutayarisha kila mahali kwa kurudi kwa Bwana (**aya 1)**

Watenda kazi kwa mavuno. Kwanini twastahili kuimarisha kanisa kila mahali? Kwa maana Yesu alisema, "***Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi muombeni Bwana wa mavuno awapeleke watenda kazi katika mavuno yake"*** **(aya 2)**

Upinzani kwa wingi. Yesu alisema anawatuma kama wana-kondoo kati ya mbwa-mwitu **(aya3).** Kutakuwa na mbwa-mwitu jihadharini! Hamtakuwa shupavu mnapotoka kwenda kupanda kanisa katika kila eneo. Unaweza kukutana na upinzani kutoka makanisa mengine yalioimarika yakiwepo, na kwa roho mbaya katika maeneo yanayo tawaliwa na wachawi na dini za uongo.

Kutembea katika utiifu wa imani. Tusichukue vitu pamoja nasi lakini tutumainie Bwana Mungu atapatiana; tusipoteze mwelekeo (hapana wamishenari watalii). Yesu alisema "***Msimuamkie mtu njiani"*** **(aya 4)** Usiruhusu kuondolewa kwenye mwelekeo.

Kuongozwa kwa amani. Ingia kwa nyumba ya mtu wa amani; kwa njia ingine ambapo unapokelewa **(aya 5)**

Tafuta nyumba ya rafiki. Iwe na kubabanua: hii ni nyumba ya rafiki? Kama sio nyumba ya kirafiki usikae hapo **(aya 6)**

Hudumu kutoka nyumba hiyo. Kaa katika nyumba ya kirafiki; pokea makaribisho yao; Hudumu kutoka kwa nyumba hiyo **(aya 7)** hatupaswi kuenenda tukibisha kila mlango; kaa mahali ambapo umekaribishwa.

Mji ukahukumiwa kulingana na ukarimu wake. Mji utahukumiwa kulingana na vile unapokea wahubiri ambao Bwana anawatuma **(aya 8).**

Ponya wagonjwa na uhubiri neno. Katika nyumba ya rafiki jitoe kuwaombea wagonjwa **(aya 9).** Yesu anatuagiza tuwaponye wagonjwa na tuhubiri ufalme wa Mungu. Wengine wanaweza letwa kwa nyumba wapokee maombi ya uponyaji habari zinapoenea. Nguvu za Mungu ziko za kuponya katika nyumba hiyo! Hii inafungua nafasi ya kushuhudia kumhusu Yesu.

Hukumu huja kwa watu katika mji ambao hawajapokea muhubiri. Kunguta mavumbi ya miguu yako ya mji ule [Tedo la kiunabii la hukumu kwa kuwa hawakulipokea neno], lakini katika kuyatenda hayo onya mji juu ya hukumu ambayo inakuja **(aya 11-12).**

Kumpokea Bwana. ***"Awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi; naye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma"*** **Aya 16.** Ni wakati watu watakapo mpokea Yesu, kuamini kwa jina lake kwamba wanazaliwa mara ya pili **(Yohana 1:12).** Kama watu wakikataa mahubiri wanamkataa Bwana.Tunampokea Yesu kwa kuliamini Jina Lake. Watu watajuwa jina lake tukihubiri kumhusu.

Mamlaka juu ya shetani. Shetani na mapepo wako chini yetu. Shetani ameshindwa, Yesu alisema "***Nimemuona shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme, Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakacho tudhuru"*** **(aya 18-19).** Maisha yetu yamefichwa na Kristo ndani ya Mungu **(Wakolosai 3:3)**

Wokovu. Yesu anahimiza kwamba muujiza ule mkuu ni kuzaliwa mara ya pili, kuleta watu katika wokovu. Lengo ni kuwaona watu wakiwa wameokoka **(aya 20)**

Wokovu unakuja kupitia ufunuo kutoka kwa Mungu. Bwana anatutuma ili awaokoe watu kupitia mahubiri yetu **(aya 21-22).** Yesu anamfunua Baba kwa wale anaotaka (**Mathayo 16:17).** Watu wanaokolewa kupitia ufunuo.

Siri kufunuliwa. Injili ambayo tumepokea ni ufunuo wa siri ambayo ilikuwa imefichwa kutoka kwa watakatifu wa Agano la Kale **(aya 23-24)**

Utendaji kazi katika kanisa la nyumbani

Katika kitabu cha Matendo ya mitume tunaona kanisa likiwa limepandwa na likifanya kazi kutoka nyumba kwa nyumba. Katika fundisho hili tunatazama mambo yanayotendeka katika nyumba.

Kuwekwa kwa misingi

- Kuja kwa Roho Mtakatifu; akipatiana nguvu ya huduma na kushuhudia kama Yesu alivyo ahidi katika **Mdo 1:8 (Mdo 2:1-13)**
- Petro anahubiri Yesu, Bwana na Masihi **(aya 14-40)**
- Wasikilisaji walikatwa mioyoni mwao kupitia mahubiri ya kusulibishwa kwa Yesu, kufa na kufufuka kwake **(Aya 37).**
- Petro anawaambia jinsi ya kuokoka; tubu na uamini neno la Bwana, na "***Walilipokea neno kwa furaha"*** mbatizwe; mpokee Roho Mtakatifu **(aya 38-41)**
  Misingi ya kanisa jipya inawekwa na mitume.

Mambo matano yanayofanya kazi katika maisha ya kanisa

Mdo 2:42 Inafunua mambo matano ya maisha ya kanisa

1. **Walidumu –** Hii inamaanisha hivyo: Waamini wa kwanza walidumu kwakujitoa au kudumu katika mambo haya mengine manne. Bila kuendelea kikamilifu kwa kujipatiana kwa mambo ya imani, kanisa halitatimiza kusudi lake
2. **Mafundisho ya kitume:** Mafundisho ya ufunuo yakiletwa na mitume.
3. **Ushirika:** Kujipatiana katika kushiriki kwa kanisa la kwanza ambapo mahitaji ya kila mmoja yalishugulikiwa.
4. **Kumega mkate:** Meza ya ushirika
5. **Maombi:** Maombi ya kila siku

Matokeo ya kudumu katika mambo ya muhimu ya maisha ya kanisa

a) **Aya 43** Hofu kubwa ikawa juu ya waamini wote. 'Hofu' hii ni hofu ya Bwana, ambayo katika agano la kale ni sawa na imani. Ishara kuu na miujiza zilitendwa na mitume. Hofu [imani] iliachilia miujiza.
b) **Aya 44** Waamini walikuwa pamoja na kushiriki vitu vyote pamoja. Jamii ya kweli ikainuka
c) **Aya 45** Mali na vitu ziliuzwa, na kilicho patikana kutumika kushugulikia mahitaji katika jamii.
d) **Aya 46** Kila siku – wakaendelea kila siku
    - Kwa kusudi moja – kwa kukubaliana, bila mambo ya kando **[sura 5:1-11]**
    - Katika Hekalu – walionekana wameshikamana, watu walio jipatiana
    - Katika ushirika wa kanisa siku zao
    - Katika manyumba

Waliumega mkate kutoka nyumba kwa nyumba, "mwana kondoo kwa kila nyumba"
Kumega mkate ilikuwa ya muhimu katika kanisa la nyumbani.
Walishiriki vyakula vyao kwa furaha na wepesi wa mioyo.

Makanisa mengi yanaruhusu mikutano ya nyumbani, lakini hawaruhusu kumega mkate. Mpaka wakati utawala wote (mafundisho ya wanikolai) yaondolewe kutoka kwa waamini, na kukutanika kila siku, kutimiza mambo haya matano ya kimsingi, hatutauhisi "upendo wetu wa kwanza" kwa Yesu na kuyatimiza mapenzi yake yaliokubaliwa.

e) **Aya 47** "***Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliookoka".*** Bwana akalizidisha kanisa, kila siku, wale waliohitaji kuokoka.

Tabia za kanisa la nyumbani katika kitabu cha matendo ya mitume

i. **Walikuwa wakiomba usiku. "*Hata walipofunguliwa, wakaenda kwa watu wao, wakawapasha habari ya mambo yote waliyoambiwa na wakuu wa makuhani na wazee"* Mdo 4:23.** Petro na Yohana wakaeneda kwa ndugu zao na wakawapasha habari. Waliwakuta watu wao wamekutanika kwa nyumba.

ii. **Kwa moyo mmoja "*Nao waliposikia, wakampazia Mungu sauti kwa moyo mmoja"* Mdo 4:24.** waliomba pamoja.

iii. **Ujasiri uliofanywa upya: "*Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu wakanena neno la Mungu kwa ujasiri"* Mdo 4:31.** Mahali (nyumba) ambapo walikuwa wakikutana palitikiswa na wakajazwa na Roho Mtakatifu tena. Walitoka kutoka nyumba ya maombi wakihubiri kwa ujasiri.

iv. **Kila kitu kwa pamoja "*Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema yakuwa kitu cho chote alicho na cho ni mali yake"* (Mdo 4:32)** matokeo yalikuwa ni ufufuo!

Jamii ya kweli inaachilia ufufuo; wengi walitaka kujiunga.

v. **Kuhubiri kwa nguvu nyingi Mdo 4:33 "*Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote" 'nguvu nyingi'***

na '***neema nyingi'*** ilikuwa juu ya mitume. Mitume walikuwa ***wakihubiri Kristo. Yesu ndiye Lango la jamii.***

vi. **Chini ya miguu ya mitume Mdo 4:34-37** inadhihirisha kiwango cha kupatiana na kujitoa kwa ukalimu kwa wanafunzi hawa. Watu walikuwa wamejitoa kutoa pesa "***Chini ya miguu ya mitume"*** na kuwaruhusu kuzipatiana. Hii ni kanuni ya neno la Mungu.

Kila siku – hawakukoma!

"*Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kuhubiri habari njema ya Yesu kuwa ni Kristo"* **Mdo 5:42** AMEN!

Mpaka turudie muundo wa biblia na tabia ya kuhubiri na kufundisha Yesu kama Kristo katika kila nyumba ambayo inayotupokea na katika maeneo ya hadhara kama Hekalu, hatutayaona maisha hayo na kushuhudia utukufu wa Kristo Yesu ambayo tunatamani. Tungali tunapatiana kibali nusu kwa kanisa la nyumbani. Makanisa mengi yanakataza kumega mkate nyumbani ila hali hapo ndipo pahali pazuri pa kumega mkate. Sio biblia wala haiwezekani kumega mkate katika kikundi kikubwa.

Kazi ya injili inaendelea, kwa hadhala na kutoka nyumba kwa nyumba kila siku.

Wazee wa kanisa katika mji wanafanya kazi kwa umoja kupanda kanisa katika kila nyumba ya rafiki. Kunahitajika kuwa na nyumba ya kweli ya kiutume ambayo italeta nafsi katika kila kijiji, katika kila mji, jiji na vijiji, ili kila nafsi iunganishwe na iwekezwe na injili ya Yeu Kristo

Ushuhuda

Mapema mwaka 2003 nilikuwa kwa mji mataifa ya ng'ambo nikahubiri kwa mikutano jumapili nne. Ya kwanza ilikuwa katika maeneo ya mashambani ambapo kulikuwa na umaskini mwingi. Ilikuwa ni ushirika mdogo kanisa la nyumbani ambapo ilihusisha kumega mkate. Nafsi tatu ziliokolewa katika mkutano huo. Niliwaelekeza kwa Bwana kabla ya kuhudumu meza. Kisha wakashiriki katika meza.

Mkutano huo mwingine ulifanyika ghorofani kwa nyumba kubwa ambayo inatumika kwa mikutano. Kulikuwa na mikutano kila jumapili na ushirika mahali hapo. Hakuna aliyekuja kwa wokovu. Mkutano wa tatu ulifanyika katika jengo ndogo la kanisa, ilikuwa imejaa na hakukuwa na meza wala aliye kuja katika wokovu. Mkutano wa nne ulikuwa wa jioni katika jengo la kanisa la Pentekote, iliyokuwa na watu 3 – 400 wakihudhulia. Mara tena hapakuwa na meza ya Bwana wala mtu aliyepokea wokovu.

Mkutano wa kwanza ulifanyika katika mazingila duni katika mtaa duni na watu wasiookoka walivutiwa na mkutano. Kumega mkate kwa mazingira kama hayo ni vyepesi, yakawaida, yakupatanisha na yenye nguvu za kuokoa kama vile tulivyo shuhudia. Huko ndiko kumega mkate katika nyumba, pakiwa na mtume ili alifundishe neno katika nyumba.

Kuongezeka

Wachungaji ambao wanaongoza makundi ambayo yanakutana jumapili katika majengo ambayo yametengwa wanauwezo wa kupanda makanisa mengi ya nyumbani. Hii inamaanisha kuwafundisha viongozi na kisha kugawa makundi kukutana katika vikundi vidogo – kutoka nyumba kwa nyumba. Sizungumzii mashirika ya nyumbani au vikundi vya nyumbani lakini ile hali ya kupanda na kuimarisha kanisa nyumbani. Hakika kazi kama hiyo ni ya kiutume na lazima ifanyike kwa kusudi la kuwa mashahidi wa Injili kwa kila kiumbe. Hii ni njia ya kibiblia ya kuelekea: **Kupanda kanisa katika nyumba ya kirafiki.**

KANISA LINALOKUTANA NYUMBANI

Kanisa la agano jipya ni kanisa ambalo linakutana nyumbani. Mitume walifundisha mafundisho ya Kristo katika mikutano ya nyumbani waamini walipokutanika kila siku. Kulikuwa na mikutano ya hadhala lakini ilikuwa ya injili. Kuna kutumia ukumbi wa hadhala kama hali ya Mtume Paulo katika Efeso ambapo aliwakusanya wanafunzi kwa sababu ya mafunzo, lakini **hakuna jengo lililo 'tengwa'.**

Kulingana na maandiko katika Agano Jipya
kanisa la nyumbani ndilo msingi na kielelezo kionekanacho.

Hile hali ya mikutano ya nyumba kwa nyumba ya watakatifu ndio kielelezo cha kanisa ambalo linaonekana katika Agano Jipya, ila tu kwa mikutano ya hadhala kuhubiri na kushuhudia mahali kama ukumbi wa Sulemani **(Mdo 5:12),** na shule ya mafundisho ya kiutume kama ile shule ya Tylano katika Efeso **(Mdo 19:9-10).**

Kusudi la huduma ya kanisa la nyumbani

Inaelezea sawa na vyepesi: Kusudi la huduma katika nyumba ni kupanda kanisa la kibiblia na kuachilia lifanye kazi. Hii ndio njia ya huduma ambayo Yesu alielekeza mashahidi sabini katika Luka; walikuwa wakae kwa nyumba ya mtu wa amani [nyumba ya kirafiki ambapo walikaribishwa], ponya wagonjwa na hubiri ufalme wa Mungu. Hawakuwa waenende kutoka nyumba kwa nyumba bali matarajio ya Yesu yalikuwa kwamba wagonjwa na waliopotea wangevutwa kwa nyumba ambapo wahuduma walikuwa wakihudumu injili walikuwa (**Luka10:1-9)**

Kanisa la nyumbani katika kitabu cha matendo ya mitume

Kuna mifano ya maandiko kadhaa katika kitabu cha **Mdo** juu ya kanisa la nyumbani.

Katika **Mdo 1:12-26** wale mia na ishirini walikuwa wakingonjea katika chumba cha juu, wakiendelea na maombi mpaka Roho Mtaktifu akaja – **walikuwa katika nyumba**.

Katika **Mdo 2:42-47** baada ya mahubiri ya hadhala katika mitaa siku ya pentekote, nafsi elfu tatu zilibatizwa na kuongezeka pamoja na wale waamini mia na ishirini. Hao elfu tatu mia moja na ishirini walikutana wapi? **Aya 46** "***Na siku zote kwa moyo mmoja, wakimega mkate nyumba kwa nyumba"* walikutana katika nyumba nyingi**. Mtu anaweza kufikiria kwamba chumba cha juu katika **Mdo 1** pengine palikuwa na watu zaidi ya mia na ishirini, **(120).** Waamini wengine walizifungua nyumba zao, wakiwakaribisha vikundi vya waamini wapya, ambao walikuwa wamebatizwa na kupokea Roho Mtakatifu siku ile ambayo waliamini, kuja kwa mikutano ambapo mitume walikuwa wakifundisha kila siku. Vile vile palikuwa na maombi ya kila siku katika ukumbi wa Suleimani (**Mdo 5:12).**

Mdo 4:23,31: Baada ya Petro na Yohana kufunguliwa na kikundi cha viongozi "***waliwaendea watu wao" [***tunaweza kufikiria walienda kwa nyumba] na kumuomba Bwana kwa sababu ya hali yao na kumuuliza Bwana ujasiri na ishara na miujiza.

Mdo 5:42 ***"Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema ya Yesu kuwa ni Kristo".*** **Mdo 9:11-19** Sauli "***alikuwa katika nyumba ya Yuda katika njia iitwayo nyofu".*** Paulo aliponywa, akajazwa na Roho Mtakatifu na akabatizwa na Anania katika nyumba.

Mdo 9:33-34: Petro alimfufua mtu aliyekuwa amepooza **kutoka kwa kitanda chake –** Tunakisia ilikuwa ni kwa nyumba.

Mdo 10:24-48: Korinelio aliwakusanya watu wake wote wa jamii na marafiki kwa nyumba yake kusikia Petro akishiriki ujumbe wa Yesu Kristo. "***Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia neno hilo"*** **aya 44.** Kisha petro akaamuru wabatizwe [nilazima iwe walikuwa na maji kwa nyumba – pengine bafu ya Kirumi!] na akakaa nao siku chache kwa nyumba akiwahudumia.

Mdo 12:12: Wakati malaika alimkomboa Petro kutoka ngereza **alienda kwa nyumba ya Yohana Mariko "*ambapo wengi walikutanika wakiomba"***

Mdo 16:15-40 Lydia aliokoka kupitia mahubiri ya Paulo na punde baada yake kubatizwa akamshawishi Paulo na kikundi chake kwamba "***mje kwa nyumba yangu na mukae*".** Kanisa **katika philipi lilipandwa kwa nyumba ya Lydia.** Hapo ndipo kanisa lilikuwa likikutana. Wakati Paulo na Sila waliachiliwa walienda nyumbani kwa Lydia ambapo walikutana na **wapendwa (aya 40)**

Katika **Mdo 16:33-34,** Yule mlinzi wa gereza na jamii yake waliokoka wote na mara wakabatizwa; kisha akawaleta mitume kwa nyumba yake na akawaandalia chakula. Tena kazi na huduma ya maisha ya kanisa ilitendeka kwa mazingila ya nyumba.

Mdo 18:7-8 Katika Korintho, Paulo alishuhudia katika Sunagogi lakini upinzani ulipoanza, "***Akaondoka huko akaingia katika nyumba ya mtu mmoja jina lake Tito Yusto, mcha Mungu, ambaye nyumba yake ilikuwa mpaka mmoja na sinagogi. Na Krispo mkuu wa sinagogi, akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote."*** Mara kwa mara katika Agano Jipya uinjilisti ulifikia nyumba yote; hii ni kwa sababu huduma ya injili ilikuja kwa nyumba!

Mdo 20:20 Paulo anashuhudia yakuwa katika Efeso "***Nilifunza wazi wazi na nyumba kwa nyumba".*** Alikuwa anawanenea wazee kutoka kanisa la Efeso. Wakati Paulo alipokuwa Efeso alifundisha wazi wazi, kila siku, katika shule ya Tylano. Lakini kanisa lilikuwa linakutana manyumbani na kwa hivyo Jioni Paulo alihudumu kutoka nyumba kwa nyumba. Shule ya Tylano ni kielelezo cha shule za mafundisho ya kiutume.

Mdo 21:8 Wakati Paulo na kikundi chake walifika Kaisaria, ***"Aliingia nyumba ya Philipo muhubiri wa injili aliyekuwa mmoja wa wale saba tukakaa naye".*** Mikutano ya nyumbani ilifanyika kiajabu na Agambo nabii alipofika kutoka Judea alihudumu kutoka kwa nyumba **(aya 10-14**).

Mdo 28:30-31 "*Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimuendea, akiwahubiria habari za ufalme wa Mungu, na kufundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu yeyote".* Paulo alikuwa ametumia miaka miwili akifundisha katika shule ya kiutume katika Efeso, lakini amejipatiana katika kufundisha fundisho la kiutume katika nyumba yake ya kupanga kwa miaka miwili. Hii ndiyo picha ya mwisho tuliyonayo ya mtume mkuu Paulo katika maandiko na alikuwa akiendelea na kanisa la nyumbani. Tumetazama maandiko yote ambayo yanaongea juu ya kanisa la nyumbani na jinsi linatenda kazi katika kitabu cha Matendo ya mitume.

Kuna kutajwa kwingine kwingi ambako hakujaonyeshwa wazi **kwa maana mikutano ya kikanisa yote na utendaji maisha ilifanyika nyumbani kuanzia wokovu, ikihusisha ubatizo wa maji kwa hekima ya ndani ya neno la Mungu ikifundishwa na mitume**

Huduma ya kanisa katika nyaraka

Warumi 16:5 "*Vile vile na walio katika nyumba yao"* [philiska na Akila]

Aya 10*: "Nisalimie watuwa nyumbani mwa Aristobuo"*

Aya 11*: "Nisalimieni watu wa nyumbani mwa Narkiso, walio katika Bwana"*

Aya 14*: "Nisalimieni Asinkrito…na ndugu walio pamoja nao"*

Aya 15*:* Kikundi kingine cha watakatifu wako pamoja na ndugu wengine ambao Paulo anawajua kwa majina.

Paulo hakuwa amefika Rumi alipo andika barua lakini anawajua ndugu katika nyumba kadhaa '**kanisa katika nyumba' wandugu pamoja'.** Kuna vikundi vitano vilivyotajwa na ni akili kuamini kulikuwa na kanisa tano za nyumbani ambao walikuwa sehemu ya kanisa la Rumi.

1Wakorintho 16:15 inataja juu ya **nyumba ya Stefana** "***Ambao wamejitia katika kazi ya huduma ya watakatifu".*** Stefana anatajwa kama muhuduma na mtendakazi pamoja na Paulo. Alihudumu kupitia kanisa ambalo lilikuwa nyumbani mwake na vile vile kusafiri katika huduma. Katika **aya 19** Priska na Akila walikuwa na kanisa nyumbani mwao katika Efesa, na pia Rumi baadaye na katika Korintho.

Katika **Wakolosai 4:15** kanisa liko katika nyumba ya Nimfa.

Philemona (1-2) alikaribisha na akaliongoza kanisa kwa nyumba yake. Alijulikana kwa upendo wake na imani na huduma yake ya kuburudisha watakatifu **(4-6**) na kwa Paulo mtume **(20-22).**

Kama ilivyo katika kitabu cha Matendo ya mitume ni makanisa machache tu yaliyotajwa ambao hukutana kwa nyumba. Hata hivyo hapajatajwa katika matendo ya mitume au katika nyaraka juu ya makanisa yaliyokutana penginepo. **Niwakati wa kurejerea ukristo wa Agano Jipya kuufuata mtindo wa kiutume kama ilivyo katika maandiko.**

Kama ilivyo andikwa

Mitume katika agano jipya wanahudumu kihadhala na kutoka nyumba kwa nyumba. Mikutano ya hadhala ilikuwa tu ni ya injili, lakini ilihusisha kunena kwa sinagogi mara kwa mara miaka ya kwanza ya kanisa na pia katika ukumbi wa hekalu. Mikutano ya maombi ilifanyika kwa maeneo ya hekalu. Hata hivyo **maisha ya kawaida ya kanisa yaliendeshwa manyumbani kutoka nyumba kwa nyumba.** Waamini wapya waliopatikana kwa njia ya injili walipokelewa kanisani na kanisa lilikuwa likikutana kwa nyumba tofauti tofauti. Wale elfu tatu waliookoka siku ya pentekote walijiunga na wale mia na ishirini, na waliendelea kukutana katika nyumba nyingi kila siku, na waliongezeka kila siku "***Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa" Mdo 2:47***

Mahali palipotajwa tu pa mikutano ya kanisa katika maandiko ni katika nyumba. Ndio, kushuhudia kihadhala kulitendeka katika maeneo mbali mbali, lakini haijatanja kwamba kanisa lilikutana katika maeneo haya kwa maisha ya kawaida ya kanisa. **Maisha ya kawaida ya kanisa, ambayo yanatendeka au kuendeshwa ya kanisa bila ubishi yalikuwa ni nyumbani.** Mbona kuna kutatanikiwa kwingi hivyo leo? Mara nyingi ninapo taja kwa wahuduma wengine juu ya kuendelea na kubuniwa kwa kanisa la nyumbani, wanajibu, '*Oh, kikundi kikiongezeka kitapata jengo.'* lahasha lengo sio hilo. Lengo ni kuongezeka kwa wanafunzi maradufu ambao wanakutana manyumbani kusikiza mafundisho ya kiutume, kushirikiana pamoja na kukutana na mahitaji ya wengine, kumega mkate mara kwa mara kama kila juma na kuomba pamoja kutambua kusudi la Bwana siku baada ya nyingine; kuwalea waamini wapya na kuwafanya waumini kuwa wanafunzi.

Utendaji kazi ya huduma katika nyumba

Katika kanisa linalo kutana nyumbani kuna

- **Maombi, ambayo inawezesha waliopotea kumpata Yesu, sifa na ibada,**
- **Ushirika na kushirikiana,**

- **Mafundisho ya kiutume – ikielekea kwa mafundisho safi, ufunuo ukifahamika na neema ikipokelewa.**
- **Fulsa nyingi za huduma – ishara na maajabu, kuhubiri na kufundisha**

<u>Yote haya yanaelezwa katika</u> Mdo 2:42-47:

Mdo 2:42 ***"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali"***

Huduma tano zilifanyika katika nyumba. Mitume walikuja kwa mikutano na kuleta mafundisho; waamini walishiriki, wakaumega mkate na kuomba pamoja. Kazi hizi nne ni za msingi katika utendaji kazi wa kanisa katika nyumba. Hata wakristo ambao wamekomaa wangali wanategemea wale wafanyi kazi wa kanisa la pale pale, hawajakabidhiwa kufanya kazi katika huduma nyumbani kumega mkate, kuomba na kujifundisha neno.

Aya 43 ***"Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume"*** Palikuwa na uhakika wa ufalme wa Mungu kati yao. Wagonjwa waliponywa; miujiza ilikuwa ikitendeka nyumbani.

Aya 44-45 ***"Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja"*** Ushirika unaokuwa kutoka kwa huduma ya msingi wa nyumba inapelekea kushirikiana kwa hali ya juu. Kila mtu aliye kwa kikundi anajulikana na kutambuliwa; mahitaji ya kibinafsi yanashugulikiwa wazi wazi na kuombewa, masaidiano, misaada na kushugulikiwa zinafuata kama vile Bwana anaongoza.

Aya 46 ***"Na siku zote kwa moyo mmoja … wakiumega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na moyo mweupe"*** palikuwa na fulsa ya waamini kukutana kila siku kwa nyumba kwa njia ya kirafiki, kushiriki chakula pamoja na kushiriki nafasi za ujuzi ndani ya Bwana katika kuumega mkate. Kumega mkate katika maandiko tangu ianze katika chakula cha mwisho ilikuwa kila mara ni katika mazingila ya chakula. Leo kanisa linaporejelea mikutano ya nyumba kumega mkate inaweza kuwa ni sehemu ya chakula cha ushirika na iwe na maana kubwa sana.

Aya 47 ***"Wakimsifu Mungu, na kupendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokoka"*** Pahali pa sifa na kuabudu ni katika mikutano ya nyumbani. Kanisa lenye msingi wa nyumba ni ya 'kiasiri' mnajuana na majilani na wale wote wanaokaa katika mazingila hayo ya nyumbani. Kanisa la kwanza lilikuwa na '***kibari na watu wote'*** – hii inamaanisha walifahamika na kuwazwa vema. Majilani wanajiunga vyepesi na kanisa la nyumbani.

Ushuhuda wa maandiko uko wazi

Kanisa la Agano jipya lilikutana kwa nyumba. Kanisa lilipandwa katika kila nyumba ya rafiki. **Mdo 5:42** "***Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo."*** Katika **Luka 10,** Yesu alituma mashahidi wawili wawili katika kila mji na mahali alipotaka kwenda. Aliwaagiza kutafuta nyumba ya rafiki na wahudumu kutoka hapo, wakiwaponya wagonjwa na wakihubiri ufalme wa Mungu.

<u>Lengo ni</u>:

- Makanisa mengi yapandwe: katika jamii ya kila Mkristo; kanisa katika nyumba ya kila mkristo, kanisa katika kila jengo, kila mtaa, kanisa katika kila shamba.
- Ili injili ihubiriwe kikamilifu; ili utume mkuu utimizwe; ili kanisa liandaliwe kwa sababu ya kurundi kwa Bwana.

- Kunatakiwa kuwe na kanisa lenye msingi wa kibiblia, lenye kufikia nafsi, lenye kujazwa Roho Mtakatifu, katika kila kikundi cha watu, ili kila nafsi ifikiwe kwa injili ya Yesu Kristo.

Kuhudu kutoka nyumba kwa nyumba

Kwa miaka kadhaa sasa Mungu ametupa mtazamo wa **Kupanda kanisa "katika kila nyumba ya kirafiki".** Maagizo ya Bwana kwa kanisa kwa wale sabini ambao alituma ilikuwa ni watafute nyumba ambapo walipokelewa na kuwaponya wagonjwa na kuhubiri injili kwa nyumba hiyo. Katika kitabu cha **matendo** na maeneo kadhaa katika **nyaraka** tunaona kutajwa kwa kanisa likikutana nyumbani. **Hakika nyumba zilikuwa ndio maeneo na mahali pa pekee ambapo kanisa lilikutana.** Majengo ya kanisa yaliyo wekwa wakfu hayakuonekana mpaka baada ya Agano jipya kuandikwa. Ni vingumu sana watu wa kisasa kufahamu kanisa lilifanya kazi namna gani mwanzo kwa kuwa muundo wa kanisa la leo ni tofauti sana. Hata hivyo **kumekuwa na kuendelea kwa urejesho wa kanisa la nyumbani.**

Mwisho wa 2005, kikundi cha kwetu kilichukuliwa na mchungaji wa kiutume ambaye yuko katika mji mdogo ambao una mitaa sita [jiji moja, miji minne na sahemu ya ukulima]. Mikutano ilikuwa na mtu mmoja katika shamba na kusanyiko la watu kumi na tano ilikuwa ndilo kubwa sana. Hata hivyo Bwana aliachilia neno lake kwa njia spesheli na kulikuwa na upako wa ufunuo na ufahamu. Tulishangaa kuona Bwana akifanya kazi tulipoenda '**kutoka nyumba kwa nyumba' kushiriki neno la Mungu na kuyahudumia mahitaji ya watu wa Mungu.**

Tumeona utendaji kazi wa ufufuo katika siku zetu, sio kwa wakati huu kukiwa na watu wengi wakiwa wameokolewa, lakini watakatifu wakiwa na **maisha yaliyo badirika** tunapoongea juu ya ufunuo wa kiutume na roho ya uwana. Mungu anatuwezesha kuhudumia watu binafsi na vikundi vidogo, ambao '**wanajifunza kuwa kanisa'** ambao hawategemei juu ya miundo au mipangilio au mielekeo iliyo wekwa ya ibaba, lakini wanao shiriki kuongozwa na Roho Mtakatifu, ambao wanachukuwa majukumu kuwa wanafunzi, kukuwa katika ufahamu wa neno. **Katika haya Bwana anatayarisha watu ambao watawafikia wengi siku zijazo.**

Katika SHILOH mwisho wa juma tunaona vikundi kutoka SHILOH zikiondoka kwenda kuhudumu katika nyumba mbali mbali. Kwa mfano, kwa juma moja wachungaji wetu wawili walitembelea kanisa la nyumbani katika Tamworth na Dorrio [miji hii miwili iko masaa sita kutoka mahali tuko] na kutembelea watakatifu katika mji mwingine – walikuwa nje kwa siku tano. Wengine waliendesha gari 200kms, na kuhudumu katika mahali katika eneo lililotengwa. Jamii nyingine za wachungaji walihudumu katika kanisa la nyumbani katika mji kwa jumapili zilizofuatana. Mungu anazidi kufungua milango kwa huduma ya kiutume katika nyumba kwa nyumba na kanisa linapandwa katika nyumba likifanya kazi kwa jia ya kimaandiko.

Kukuwa katika jamii ya Kikristo

Mwisho wa mwaka wa 2005 kikundi cha watu wanne kutoka kikundi cha kitume cha SHILOH kilitumia majuma mawili na nusu wakiishi katika jamii za wakristo katika taifa letu ambapo idadi yake ni kama waislamu wote na wakristo walioko kama asilimia tatu ni wakristo wa kawaida wakiwa wametoka kwa dini ya kitamaduni. Vitengo vyote vya Kikristo viko katika taifa hili, pamoja na vikundi ambavyo hatujavisikia mbeleni.

Katika mazingila kama haya Mungu analiinua kanisa la siku za mwisho. Pentekote wamekuwa wakihubiri injili na kufaulu kuyapanda makanisa machache. Hata hivyo sasa kuna **baadhi ya viongozi wachanga miongoni mwa wapentekote ambao wana moyo wa urejesho wa kiutume kamili na kufanywa upya kwa kanisa.** Tayari kazi yao mashinani haijaonekana

wanapotoka kwa msingi wa jamii ambapo baadhi ya watu wa jamii na ukoo wamejipatiana kikamilifu kwa kazi ya huduma ambayo wachungaji hawa wanafanya. Tulitunukiwa fulsa ya kuishi katika jamii hizi!

Kila kiungo kikifanya kazi

Tuliishi katika mazingila ya jamii kubwa ya wakristo ikihusisha vijana waliooa na jamii zao na watu wengine walio karibu wa ukoo. **Jamii hii kubwa imejipatiana katika kuimarishwa kwa ufalme wa Mungu: Wengine wanatoka kuenda kazi, mmoja wa wandugu ni mfanyi biashara aliyefaulu, na wote wanachangia kifedha kwa kazi ya huduma.** Mwana ambaye ni mchungaji anaheshimiwa na jamii yote kama mtu wa Mungu na wote wanahusika na kazi ya huduma. Vile vile, watenda kazi wengine, ambao hawaishi katika mazingila hayo, wanahusika kikamilifu katika huduma.

Mazingila haya ya kikristo yako miongoni mwa mkoa wa waislamu lakini jamii hii inatambulika. Wanapata kibali katika biashara wakati wanabiashara waislamu wanapokuja nyumbani kuulizia. Pia majilani wanakuja kwa maombi na wanakuja kushuhudia yale Bwana ametenda baada ya maombi. Kupitia kupatana na mfanyi kazi Muislamu tulipokea usafiri na katika tukio moja tukakaribishwa katika Hoteli moja kwa chakula cha kirafiki.

Kanisa katika nyumba

Jamii hii kubwa wakiwa na wengine wengi wakiishi pamoja na wakifanya kazi pamoja kwa upanuzi wa huduma, walikuwa tayari kufanyika **kanisa la nyumbani, na viongozi wa kikundi cha kiutume kinachochipuka.** Katika jumapili ya pili saa nane, watu wa jamii na wengine waliosaidia huduma ya ndugu wetu, walikusanyika na jamii yote na tukawa na wakati waajabu sana wa ‘kanisa la nyumbani’ tukikutana na zaidi ya watu sitini wakiketi katika sakafu ya pahali tulipokutania.

Huu ulikuwa ni ujuzi mpya kwa wapendwa hawa kwa maana walikuwa mwanzo wamehusishwa na ‘kanisa’ kwa mikutano mingi katika jengo lililotengwa, hata kama kupandwa kwa kanisa kwao ni katika mazingila ya maeneo ya nyumba, moja wapo ya mambo yaliohimizwa katika kanisa la nyumba ilikuwa ni **Kumega mkate na ikihusisha jamii yote katika sherehe hizi na Bwana Yesu Kristo.** Kwa njia nyingi mikutano hii ya nyumbani ilihimizwa kwa maana ilionyesha **Kurejeshwa kwa kanisa la kiutume, linalo rejeshwa na kukutana kwa nyumba.**

Jambo la kutazama

Tangu tuanze Revival Minisry katika mwaka wa 1998 tumekuwa tumejipatiana katika kupanda makanisa ya nyumbani. Tulitambua kuanzia mwanzo kwamba ‘**sisi ni kanisa’** na Mungu akatuonyesha kuzifanya ‘**kazi za kwanza’** kulingana na **Mdo 2:42**. Hizi tulifanya kila mahali tulipokwenda hata katika ndege tuliposafiri katika mataifa.

Tulihimiza kukutana manyumbani kila tulipoenda na kwa miaka kadhaa tumetembea Australia, tumekaribishwa katika nyumba nyingi lakini sio majengo mengi ya kanisa.
Mapema mwaka wa 2007, tuliwauliza wandugu waliokuwa wakikutana jumapili kwa mikutano katika kituo cha SHILOH wajigawe katika vikundi vidogo na wakutane katika kanisa la nyumbani. Tulikuwa na makanisa mawili ya nyumba yaliyokuwa yanakutana jumapili katika maeneo ya mashambani nje ya mji wa Toowoomba, lakini kuanzia January makanisa mengine matatu yalikutanika katika mji. Moja wapo wa vikundi hivi wanaendelea kukutana katika kituo cha SHILOH lakini wanaketi kwa mviringo chini ya ghorofa.

Jumapili moja kwa mwezi hivi vikundi vitano wanakutanika **kwa ibada ya jamii kusherehekea.** Katika mwisho wa juma hilo tunakuwa na usiku wa ijumaa maalum tukikutana na

kuabudu na wakati wa kumngojea Mungu na kwa jumamosi hiyo inakuwa ni siku ya kujifundisha kuanzia 10:00am hadi 4:00pm. Wandugu kutoka maeneo ya karibu na waliotoka mbali, wanajumuika nasi katika mwisho huo spesheli wa juma na zimekuwa zina umuhimu mkubwa sana kwetu kwa maisha ya kanisa.

Sababu zilizotufanya tufanye badiliko la msingi wa nyumbani kutoka mkutano wa kusanyiko hadi makanisa ya nyumbani zilikuwa kama ifuatavyo:

- Kushamazisha **uwajibikaji wa kila mtakatifu binafsi awe mtu wa kiungo kinacho husika katika** mikutano ya kanisa (**1Wakorintho 14:26)**
- Kuhimiza kila mtakatifu binafsi au jamii **kuwajibika kwa mahitaji ya washiriki wengine** wa kanisa la nyumbani.
- Kumpa kila mshiriki **hile hali ya umiliki**: 'Hili ni kanisa langu na ninawajibika kwa ufanisi wake'.

Kukutana katika vikundi vidogo

a) Inawezesha mtu binafsi kufanyisha vipawa kazi na kuchangia katika mikutano.
b) Inahimiza wandugu kuanza kushugulikiana kikundi chote kinapofanya kazi kama jamii.
c) Inachangia kuinuliwa na kufundishwa kwa viongozi wapya, ikipatiana nafasi kwa watu wanaojifunza wapate ujuzi.

KANISA LA SIKU YA TATU

Mnamo mwezi wa nane mwaka wa 2005, nabii alishiriki neno kwetu SHILOH lenye kichwa, '**kanisa la siku ya tatu.'** Hii ndio iliyokuwa siku ya kwanza ya kusikia mafundisho ya kanisa la siku ya tatu. Kwa kipindi cha miezi tisa tulikuwa tumesikia mafundisho mengine mawili ya kanisa la siku ya tatu kwa wageni waliotutembelea SHILOH.

Maandiko yaliyotumika haswa yalikuwa **Hosea 6:2** ***"Baada ya siku mbili atatufufua, siku ya tatu atatuinua, nasi tutakaa mbele zake"*** na **Luka 13:32** ***"Akawaambia, nendeni, mkamwambie yule mbweha, tazama leo na kesho natoa pepo na kuponya wagonjwa, siku ya tatu nakamilika".*** Hii inaeleweka kiunabii kama utawala wa miaka elfu moja ambayo inalinganishwa na miaka 1000 kwa kila mwaka. Kutoka Adamu mpaka Kristo ni karibu miaka 4000 na tangu wakati wa kifo cha Kristo mpaka sasa ni karibu miaka 2000 za kuja kwake na hivyo utawala wake na umiliki wa Kristo duniani na watakatifu wake miaka 1000. Mungu anaharakisha kazi yake katika siku zetu kwa maana kutakuwa na watu wa kifalme, makuhani wa mpangilio wa Melkizedeki, wakitembea katika ukomavu, wakifanyika kanisa lenye utukufu ambalo Yesu anajitayarishia.

Asili tatu za asiri ya ufunuo unaofunguka

Kwa miaka Mungu amekuwa akifunua asili ya ufunuo wa asiri tatu kwa ufunuo unaofunuka katika kukabiliana na mwanadamu, kutuleta katika kutembea katika ukomavu tunapoingia na kuhisi ngazi ya tatu. Hii imeonyeshwa katika mafundisho ya ufunuo wa Hema ya Musa.

Hema ya Musa:

- Sehemu ya nje, ambayo inaweza semwa kuwa ni ujuzi wa kanisa la siku ya kwanza; **Yesu** ametuokoa kutoka ulimwenguni, katika hali ya kutimiza sehemu ya nje [madhabahu ya sadaka ya damu na maji = wokovu ikihusisha ubatizo wa maji].

- Pahali patakatifu, ambayo yaweza semwa kuwa ni ujuzi wa kanisa la siku ya pili; Yesu **ametubatiza na Roho Mtakatifu** akituleta katika ujuzi wa pahali patakatifu ambapo tunajifundisha kuhudumu mbele ya Mungu.

- Kuingia ndani ya pasia patakatifu pa watakatifu ambao ni ufunuo wa kanisa la siku ya tatu; hatimaye Yesu anatuleta ndani ya pasia katika uwepo wa utimilifu wa utukufu wa Baba, Hii ndiyo hatima Yetu!

Waebrania 9:1-5 Kwa kifupi inaeleza Hema ya Musa, lakini katika hayo inatujulisha ufunuo mkubwa. **Aya 2** inatuambia kwamba chumba cha kwanza cha hema, kinachoitwa madhabahu, au pahali patakatifu, kuna kinara na meza ya mkate wa uonyesho lakini haitaji chombo hicho kingine cha mbao ambacho kilikuwa pahali patakatifu, chekezo cha dhahabu. Tena maandiko inasema kwamba kado na saduku la agano 'chekezo' cha dhahabu ilikuwa katika patakatifu pa watakatifu (aya 3,4). Hata hivyo maneno ya kiyunani **SC#2369** Ni '*thumiasterion' na kiasiri inamaanisha pahali pa moshi pa kuharibu kile kisicho takikana, hiyo ni madhabahu ya uvumba* . Lakini imetafsiliwa chekezo. Hakika hii ni kutoeleza kwa njia nzuri.

Madhabahu ya uvumba

Madhabahu ya uvumba kilikuwa ni chombo cha muhimu ambacho kilipatianwa na Mungu katika Hema. Mwanzo kilikuwa kimewekwa nje ya pasia kando ya Saduku la Agano. Katika Agano jipya sasa kinasemwa kuwa katika Patakatifu pa watakatifu. Haya yanawezekana aje, na je huu ni ukweli wa ndani ambao Roho Mtakatifu anatufunulia? Kupitia kifo cha Yesu pasia imeondolewa na tunapaingia patakatifu pa watakatifu kwa ujasili "***kupitia mwili wake"*** (**Waebrania 10:20).** Sasa pasia haipo tena kuigawa sehemu moja ya nyumba ya Bwana, ikimaanisha ya kuwa tunaweza kukikaribia **kiti chake cha enzi cha neema**! **(Waebrania 4:16)**

Zile sikukuu tatu za Waisraeli

Ufunuo na ufahamu wa sikukuu za Waisraeli unatuwezesha kuingia katika ujuzi wa sherehe ya tatu na kutembea katika ukomavu hadi ukamilifu.

- **Pasaka** katika sehemu zake tatu: Siku ya pasaka, Sikukuu ya mkate usio tiwa chachu na siku ya Malibuko, imetimizwa na Yesu kufa msarabani na kufufuka tena na inatimizwa katika maisha ya muamini kupitia **wokovu na pia ubatizo**.

- **Pentekote,** neno la Kiyunani ya sikukuu ya majuma, sikukuu ya siku moja, siku 50 baada ya pasaka, imetimizwa na Yesu kumtuma **Roho Mtakatifu, kuwawezesha waamini kuhudumu kama makuhani na watumishi**

- **Sikukuu ya vibanda** Ikianzia na kumbu kumbu za kupuriza bharagumu – kuliita kanisa kutembea katika ukomavu – ikifuatwa na siku ya upatanisho ambayo inatimizwa na watakatifu kuziacha dhambi, inatuleta katika wakati wa vibanda ambayo inatimizwa katika Uungu wote ukidumu kwa watakatifu. (**Yohana 14:23, Wakolosai 2:9-10).**

Ufunuo wa Uungu

Kila sikukuu na kila kitu katika Hema inatufunulia ndani mwetu utatu wa Mungu;

- Kwanza **Yesu** anayetuokoa na tunasena ya kuwa tunamjuwa Yesu na tumekuwa wanafunzi wake, watoto wake.
- Pili Roho Mtakatifu; **Yesu** anatujaza na **Roho Mtakatifu** na tunayatambua maisha ndani ya Roho, tukifanyika wahuduma wake.
- Tatu ni Baba; lengo la mwisho ni **Yesu** kutuleta katika utimilifu wa Roho kwa **Baba**, tukipokea hali '**yakufanyika wana'**

Tatari tumekwisha kuona uwakilishaji wa hema ya Musa katika Agano jipya haijaonekana kama vyumba viwili tofauti lakini moja kwa sababu pasia imeondolewa kupitia Yesu. Kwa hivyo mwisho ufunuo wa Mungu ambao Yohana anasema kuwa akina baba wanao, ***"Wanamjuwa yeye tangia mwanzo"*** **(1Yohana 2:12, 14)** ni ufunuo wa UMOJA wa Mungu.

Kuridhi ahadi za Mungu

Picha nyingine wazi katika Agano la Kale ambayo inaonyesha kutembea kwetu ni **kutoka kwa waisraeli Misri safari katika jangwa [ya ulimwengu],** kisha **kufika na kuridhi nchi ya ahadi.** Tumeokolewa kutoka ulimwengu, lakini kama wana wa Israeli inachukua utendaji kazi wa Mungu kupitia Roho wake Mtakatifu kuuondoa ulimwengu ndani yetu – uhuisho wa nafsi zetu "**Yeye huihuisha nafsi yangu"-** ili tuwe tayari kama washindi kuingia katika uridhi wetu na kutembea na Mungu katika kutimizwa kwa ahadi zake kuu na za dhamani (**2Petro 1:2-4).**

Wengi wamefundisha kwamba uridhi au ‘nchi ya ahadi’ ni mbinguni. Hata hivyo hii ni kutoelewa ya kushangaza ya kusudi la Mungu la milele kama ilivyo fundishwa katika maandiko. Paulo anatufundisha katika **Waefeso 3:2-11** kwamba huu ni ufunuo wa siri ya Kristo na kanisa na kutimizwa kwa kusudi la Mungu; Katika **1 Wakorintho 2:6-7** Paulo anatuambia kwamba ni siri hii, hekima kwa walio komaa’, hekima iliyo fichwa’, ambayo Mungu aliweka kabla ya nyakati **kwa sababu ya utukufu wetu.**

Uridhi hauko mbinguni lakini **ni ufalme wa Mungu ukifunuliwa hapa ulimwenguni kupitia kanisa,** ukileta kutimizwa kwa ahadi za Mungu ambapo “***Dunia hii nzima itakavyo jawa na utukufu wa Bwana”* (Hesabu 14:21)** na ***“kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikavyo bahari”* (Habakuki 2:14).** Hii inafanyiwa kazi katika kudhihirishwa kwa wana wa Mungu (**Warumi 8:19)** ambayo ni “***kuwaleta wana wengi katika utukufu”* (Waebrania 2:10).** Tayari mbinguni kumejaa utukufu wa Mungu, lakini kusudi lake wazi ni kujaza ulimwengu na utukufu wake.

Watoto wadogo, vijana na akina Baba

Mtume Yohana (**1Yohana 2:12-14),** anaeleza vizazi vitatu, au vikundi vya watu, katika msingi wa ukomavu ambazo zastahili kuwa kanisani wakati wote: watoto wadogo, vijana, na akina baba.

Watoto wadogo

Watoto wadogo wanawakilisha watu wapya waliookolewa ambao wanastahili kuimarishwa katika imani kupitia kulishwa katika huduma ya uchungaji, kuwalisha na maziwa ya neno. Yesu alimwambia Petro ***“lisha kondoo wangu”* (Yohana 21:15)**

Kisha watoto hawa wanastahili kufundishwa katika neno la Mungu – mafundisho ya imani – na walimu. Yesu aliamuru ***“tufanye wanafunzi kwa mataifa wote, tukiwabatiza …tukiwafundisha kuyashika mambo yote”* (Mathayo 28:19-20).**

Lakuhuzunisha ni kwamba makanisa mengi hawajatii kuwafanya wanafunzi lakini wametosheka kuwa na ‘washiriki wengi’. Ilikuwa ni mshtuko mkuu kwa ndugu mtume rafiki yangu yakuwa alipoanza kufanya wanafunzi katika kikundi cha kanisa la pale pale, aliwapata baadhi ya washiriki ambao walikuwa hawajaokoka bado, wengine walikuwa hawajabatizwa kwa maji na wengine walikuwa hawajajazwa na Roho Mtakatifu, kumekuwa na jambo la kupuuza mafundisho ya kimsingi.

Vijana

Vijana ni wale “***wenye nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu nanyi mmemshida yule muovu”* (1 Yohana 2:14).** Vijana wanawakilisha wale ambao baada ya kupokea mafundisho ya kimsingi [kufundishwa katika neno la Mungu] na sasa wana **ushuhuda; neno linadumu ndani yao na wanamshida yule muovu**. Kwa hivyo wanaweza kuwahudumia wengine. Watu kama hao wanataka mafundisho spesheli kufundishwa na kuandaliwa kwa huduma, ili wawe watumishi katika nyumba ya Mungu, wakiuhubiri ufalme wa Mungu.

Akina Baba

Wale 'baba' ndio waliokomaa. Kumbuka “***Katika Kristo, hapana mume au mke”* (Wagalatia 3:28)** Wababa kwa kueleza wanao watoto. Matarajio ya Mungu ya kawaida ni kwamba kuwe na akina ‘baba’ kanisani, hivyo ni wababa wa kiroho na akina mama ili wawalee watoto wachanga wawe vijana ambao wanahitaji ubaba ili kuwaleta katika pahali pa ukomavu. Wakati vijana wanapofika pahali hapo pa ukomavu watapokea “***Hali ya kufanyika wana”***

(Waefeso 1:5). Ni wakati wa ukomavu [majira, wakati, sio mda fulani, 'saa' fulani] ambapo vijana wako tayari kupokea hali ya "**kufanywa wana"** ambayo ni 'kuwekwa kama mwana' wakati wa kupokea uridhi uliyoahidiwa.

Mungu amerejesha akina Baba

Kwa maana kumekuwa na upungufu wa akina baba kanisani mwa Yesu Kristo, Mungu amepatiana jawabu kwa njia ya kumtuma "***Eliya nabii, na atarejesha [anarejesha] mioya ya wakina baba kwa watoto"* (Malaki 4:5-6).** Mwisho huu Mungu ameinua mitume mwisho wa nyakati, wakija na roho na nguvu za Eliya, ni akina baba na kupitia baba wa kiutume ambapo ameinua, Mungu ameachilia ukweli na uhakika wa uwana. Hata hivyo katika uhusiano huu wa ajabu kuna kutofahamu kwingi kutoyaweka mambo vyema.

Baadhi ya mitume wamejipatiana katika kujiinulia wana na wamesisitiza umuhimu wa kuwa na baba kwa njia isio ya maandiko. Kwa asili ni watoto wanaohitaji baba, sio wana waliokomaa. Ni hivyo tu katika kiroho: ni wana katika Kristo ambao wanahitaji baba ili wafunzwe na watayarishwe ili wawe watumishi katika ufalme wa Mungu. Watumishi hao wanapo komaa wanafika kiwango ambapo wanakuwa tayari kupokea hali ya kuwa wana. Wengine hawajaona ufunuo wa 'uwana' ambayo imefundishwa wazi katika maandiko na ujuzi na uhakika kuwa uwana ni ujuzi wa Roho Mtakatifu akitimiza ile ahadi '***ili tufanywe wana kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake"* Waefeso 1: 5-6.**

Mungu pekee ndiye 'anayewapata' wana

Ambao wamefanyika wana wanahitaji ubaba ili wawe baba waliofaulu. Hata hivyo ni Mungu peke yake ambaye anaweza '**kupata**' wana. Ni utendakazi wa roho wenye nguvu sana ambapo wahuduma waliokomaa wanasema 'ni kama kuzaliwa mara ya pili' mara tena'! Wajibu wa mtume kama baba ni kuwapa ubaba wana, wawe wakina baba kwa wakina baba. Wana ambao wamepata ubaba kupitia mitume wana uwezo wa kuwalea 'vijana' ambao wanakuwa katika huduma wakiwaleta katika uwana na pia wanakuwa akina baba. Mungu anataka watoto wake wote wapokee ubaba na Mungu analeta "***wana wengi katika utukufu"*** kupitia Yesu Kristo ambaye tayari amekamirishwa kupitia mateso kwa ajiri yetu (**Waebrania 2:10)**

ELIYA ANAKUJA KWANZA NA ATAREJESHA MAMBO YOTE

"Naye akajibu, akawaambia, kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote" **Mathayo 17:11. *'Eliya alikuja'*** kupitia huduma ya Yohana mbatizaji, katika kutayarisha kuja kwa Bwana Yesu mara ya kwanza **(12-13).** Lakini Eliya astahili aje tena kurejesha mambo yote ***"kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na ya kuogofya"*** **(Malaki 4:5-6) –**kuja kwake Bwana Yesu mara ya pili.

Siku ya Bwana ya kuogofya

Tumebarikiwa kuwa tunaishi siku za kujiandaa kwa kurudi kwa Bwana Yesu mara ya pili, hata kama ni '**siku ya kuogofya'**, Ya kuogofya kwa sababu itaongezea hukumu ya Bwana wetu hapa ulimwenguni. Kikundi cha kwetu kilikuwa Pakistani mpaka mapema kidogo kabla ya tetemeko la ardhi katika mwisho wa mwaka wa 2005.

Ulikuwa ni mshituko kufahamu kwamba tuliowaendea, mimi ndiye niliyekuwa mtume halisi wa kwanza waliyempokea kule Pakistani, na kutambua kwamba maombi mengi yalifanywa, kwa Pakistani, Australia, Mauritius, Africa, Myammar na pengine kwingineko. Tulishuhudia kugandamizwa kwingi katika Taifa hilo kwa umaskini, kutatanikiwa na upinzani, na kushuku, na hali ya kutokuwa na urafiki. Kisha tukashuhudia hukumu [tetemeko la ardhi novemba 2005] ambalo liliadhiri mamilioni, zaidi ya watu 70,000 wakipoteza maisha yao. Mungu anasema wazi katika neno lake ya kwamba kusudi la hukumu ulimwenguni ni kwamba watu "***Wajue ya kuwa mimi ndiye Bwana"*** **(Ezekieli 30:19).**

Hukumu katika Kuja kwake

Kuja kwake Bwana wetu mara ya pili sehemu yake kubwa ni hukumu: wakati wa "***Kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka Mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake, katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi hao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile…"*** **2 Wathesalonike 2:7b-10**

Roho wa uwana

Sehemu muhimu katika urejesho inayoletwa na '**Eliya kurejesha mambo yote'** ni urejesho wa mioyo ya baba na urejesho wa mioyo ya watoto (**Malaki 4:6**). Neema kubwa ambayo Yesu Kristo anaachilia kwetu siku hizi ni **neema ya uwana**; neema kuu ambayo Yesu Kristo anatuachilia sisi sote katika siku hizi ni **neema ya kuwa wana**; a**naachilia roho ya kufanywa wana**, ambayo ni kuachiliwa kwa neema yake na nguvu za kutuwezesha kutembea katika uana, **kutembea katika uhusiano uliokomaa na Mungu kama Baba wetu.**

Tunakuwa "***waridhi wa Mungu na waridhi pamoja na Kristo"*** (**Warumi 8:17)** siku ile tunapozaliwa mara ya pili, lakini ni lazima tukue katika Kristo kutoka uchanga, tupitie utoto, ubarehe na ujana tukifika ukomavu, ambao ni umri wa kuwekwa pahali petu kama wana, waliokomaa, sasa tayari kuupokea uridhi ambao Mungu wetu ametuwekea.

Kupokea kwa neema hii kubwa na nguvu za kutuwezesha zinapatikana kwa wale ambao mioyo yao iko kwa Kristo katika siku za mwisho; kwa wale watakaoviacha vyote na "***Kwanza***

kuutafuta ufalme wa Mungu na haki yake" **Mathayo 6:33;** Kwa wale ambao watatoka "***Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu; Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana mwenyezi"*** **(2 Wakorintho 6:17-18).**

Twapaswa kuwa tumetengwa kwa Mungu na kusudi lake: hapana kuchaganya! Hapana kufungwa nira moja, hapana miungu moyoni, ambayo inatusongesha mbali. Hapana tena visababu ni kwa nini hatuwezi kuwa na moyo wote na mawazo yote kwa Kristo na kusudi lake.

Neema na utume

"***Kupitia yeye tumepewa neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani kwa ajili ya jina lake***" **Warumi 1:5.** Hii ni aya yenye nguvu sana ikitufunulia jinsi injili itapata ushindi katika mataifa. Mungu **ametupa neema kupitia Yesu Kristo** nani kupita **'utume'** ambapo mataifa yatafikiwa; ni kupitia uhakika na kipawa hiki Spesheli na maalum ambacho kilipatianwa kwanza na Mungu kwa kumtuma Yesu Kristo mtume wa maungamo Yetu **(Waebrania 3:1).** Kisha kalama hii ilipatianwa na Yesu Kristo katika kuaminika katika kuwainua mitume kumi na wawili: Huduma ya Agano Jipya kwa **agano jipya**, **ya msingi wa kuimarisha na kujenga kanisa la Yesu Kristo**; na pia ikapatianwa na Yesu katika kupaa kwake kupitia Roho Mtakatifu. Kwa hivyo hii neema ya kiutume inapatikana leo na ndio hakika inatakikana kanisani leo kutimiza jukumu lililopatianwa na Mungu.

KUTII = 'Kusikia chini'

Neno kuu katika **Warumi 1:5 ni** neno KUTII. Kimsingi inamaanisha 'kusikia chini'. Neno sawa na hili linatumika **2 Wakorintho 10:5** "***na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo"*** inajalisha sana **tusikiavyo** na kile **tunacho kisikia;** inahusika na maandalizi ya moyo na shauku ya ndani na ushawishi wa kumuamini na kumtafuta Mungu **(Waebrania 11:6). "*Ni kuitii imani"*** Imani huja kwa jia gani? "***imani huja kwa kusikia na kusikia kwa neno la Mungu"*** **(Warumi 10:17).**

Unasikia nini? Unachokisikia kinakuongoza kuitii imani?

Usipojiweka pahali pa kusikia mafundisho ya kiutume na kujiweka pahali pa kupokea ufunuo wa siri kutoka kwa mitume wake watakatifu na manabii (**Waefeso 3:4-5 na 8-10),** hautaweza kupokea neema ya utume ambayo Mungu amepatiana ndani na kupitia kwa Yesu Kristo. Ni neema hii ya kiutume ambayo inaleta kanisa katika kila taifa katika "***Utiifu wa imani".*** Hii ndio imani tunayo ipigania, "***Imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** (**Yuda 3**). Imani hiyo imetiwa maji au kutofundishwa mpaka wakati huu lakini Mungu amerejesha mitume na manabii kufanya kazi ya huduma, kukamirisha huduma tano ambazo Kristo alipatiana katika kupaa kwake, "***Kwa kusudi la kuwakamirisha watakatitu, … Hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapo ufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu"*** **Efe 4:12-13.**

Kutoka kwa misingi hadi ukamilifu

Misingi katika nyumba ya Mungu ni mitume na manabii (Efe 2:20). Huduma hizi mbili zinaweka msingi vizuri katika neema na kweli ya Bwana Yesu Kristo ambaye tu ndiye **msingi** (**1Wakorintho 3:11)** ambaye tunajenga juu yake. Kisha mwinjilisti anahubiri injili, akiwaleta

waamini wapya kwa kanisa ambalo limewekwa imara ambapo mchungaji na mwalimu wanahudumu, kulea na kuwafunza waamini.

Hata hivyo huduma za muchungaji na mwalimu zinaweza kuwafikisha watakatifu kiwango fulani katika ukomavu wao. Kisha mitume na manabii wanahitaji kuleta mafundisho na kuandaa kuwaleta watakatitu katika ukomavu kamili, wakitambua, kufahamu na kufundisha hekima ya ndani ya Mungu, Ufunuo wa siri.

Yesu Kristo ndiye msingi wa kanisa. Hakuna msingi mwingine ambao tunaweza kujenga juu yake. Mitume ndio wakwanza katika msingi: "***Wewe ni Petro"*** jiwe la msingi. "***Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni"* (Mathayo 16:18-19).** Hii ni ya nguvu namna gani!

Yesu kristo amepeana manabii wa Agano jipya, **waonaji, macho ya huduma tano** kufanya kazi pamoja na mitume, kuelekeza, kuonya juu ya mashimo, kubabanua upinzani, kutangaza ukweli wa siku hizi, kuongea uzima katika maisha ya watu na makanisa. Katika siku hizi Mungu anapeana kwa kila ushirika, kwa kila kanisa la pale pale, kila kanisa la nyumba kupokea misingi ya Biblia ya huduma za mitume na manabii.

Kisha kanisa linaweza kujengwa katika Kristo, Jiwe kuu la pembeni na kanisa linaweza kukuwa katika mambo yote katika kichwa ambaye ni Kristo. Haya kutendeka manabii na mitume wanahitajika ili kuleta kujenga (Kuimarisha) kwa watakatifu kuwezesha mwili wote kukuwa***, "kufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **Efe 4:12-13.**

Huduma zile zile ambazo zinapatiana msingi wa kuunganisha kwa mwamba, Kristo, sasa zinaleta kukamilisha kwa njengo la kanisa kwa kuhubiri Kristo, "***tukimuonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika Hekima yote tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo"*** **Wakolosai 1:28.**

MWANAUME MTOTO KAMPUNI

Mwanamke aliyevikwa jua

Ufunuo 12 Unatangulisha ***"Mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili" aya 1.*** Mwanamke ni nani? Kabla ya kujibu swali hii tujikumbushe ya kwamba **Ufunuo 1:1** yatuambia kwamba kitabu cha ufunuo kinafunua mambo "***ambayo kwamba hayana bundi kuwako upesi",*** hivyo ni, kutuambia mambo yatakayokuja. Mwanamke huyu anaelezwa katika kuunganishwa na sehemu za ulimwengu wote: ***"amevikwa jua".*** Katika kubadirishwa kwake uso wa Yesu ***"Ukangaa kama jua"*** **Mathayo 17:2.** Kanisa limenenwa kuwa 'bibi harusi wa Kristo' kanisa ndiye mwanamke. Mwanamke amechukua tabia za Mwana wa Mungu, Mume.

Joka jekundu ya kuogofya

Huyu mwanamke ako tayari kujifungua na katika hali hiyo "***ikaonekana ishara nyingine mbinguni na tazama, joka kubwa jekundu alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba" aya 3.*** Hapana shaka ya joka ni nani. Shetani ndiye adui mpinzani wa kanisa, kila mara akitaka kuiba kuua na kuharibu (**Yohana 10:10)**

Mtoto atazaliwa

"*Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake" aya 4.* Kuna kuzaliwa kulikotabiliwa na kuzaliwa huku kumetajwa mara nyingi katika maandiko. **Sayuni anawazaa wana wake!** Maandiko mengi katika Manabii yanazungumzia Sayuni akiwa katika utungu, akiumwa ili ajifungue. **Isaiya 66:7-10** ni moja wapo wa hiyo, "***Kabla ya hajaona utungu alizaa; kabla maumivu yake hayajampata alizaa mtoto mwanamume. … Maana Sayuni mara alipoona utungu alizaa watoto wake"*** Sayuni kiunabii anawakirisha bibi harusi wa Kristo; alijifungua mtoto mwanamume (mmoja); alijifungua watoto (wengi). Tunaweza kusema kutoka kwa haya kwamba **Mtoto mwanaume anawakilisha kikundi kikubwa kwa pamoja.**

Kufanyika wana wa Mungu

Katika **Warumi 8** paulo anazungumzia ***"viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu"*** **aya 19.** Kisha anasema ***"Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja, navyo vina utungu pamoja hata sasa. Wala si hivyo tu; ila na sisi tulio na malibuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukitazamia kufanywa wana, yaani ukombozi wa mwili wetu,…lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkika"*** **aya 22,23,26.** Kuna kuzalisha! Ni kuwaleta wana wa Mungu! Roho yuko katika kazi katika bibi harusi kanisa kufanya kitu kizaliwe: **kuzaa wana wa Mungu ambao viumbe vyote wanangoja.**

Kutawala mataifa yote na fimbo ya chuma

"*Naye akamzaa mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma"* Ufu 12:5. Nukuu hii imetolewa kutoka **Zaburi 2:7-9** ambapo Mwana ameahidiwa mataifa kama uridhi wake na "***Utawaponda kwa fimbo ya chuma, na kuwavunja kama chombo cha mfinyazi."*** Kwa sababu hii, wengine wamesema huyu mwanamke ni Maria au mwanamke ni watu wa Agano la kale ambao walimleta Masihi. Hata hivyo, kama kitabu cha ufunuo ni cha

mambo yatakayokuja ni lazima tutazame mbele na tufahamu kanisa na kuletwa kwa kikundi cha mtoto wa kiume katika siku hizi za mwisho. Kanisa la kweli limefanywa na watu waliozaliwa na Roho, waamini waliobatizwa na Roho washiriki waliobatizwa washiriki wa mwili **(1Wakorintho 12:13)**

Kumshinda Yezebeli

Ufunuo 2:18-29 ni barua ya Yesu kwa kanisa la Thiatira. Hili ni kanisa ambalo limeitwa kumshinda Yezebeli. Hapa tu ndipo ambapo Yezebeli ametajwa katika Agano Jipya lakini ni ya muhimu sana. Yesu anaahidi kwamba yule atakaye mshinda Yezebeli na "***kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa, kama vyombo vya mfinyazi vipondavyo, kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu."*** Ni ahadi hii ya kanisa lishindalo nguvu za Yezebeli ambayo inatupa ufahamu juu ya ambaye Mtoto mwanamume anawezakuwa.

Kutawala ni kuchunga

Mwanamke katika **Ufunuo 12** anajifungua mtoto mwanamume ambaye alikuwa ayatawale mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Ahadi ya Masihi katika **Zaburi 2** imepatianwa kanisani na Masihi kwa kanisa lake katika **Ufunuo 2:26-27.** Neno **'tawala'** katika **Ufunuo 2:27, 12:5 19:15,** ni neno la Kiyunani *'Poimaino,'* likimaanisha 'kutunza kama mchungaji'. Kristo anatawala kama mchungaji na watu wake watatawala na Yeye na roho ya mchungaji; '**lakini kwa fimbo ya chuma.'**

Neno la Mungu lisilobadilika

Mchungaji atachunga aje na fimbo ya chuma? Fimbo ni fimbo ya nidhamu au mwelekeo na chuma ina nguvu sana na haivujiki. Fimbo ya chuma ni neno lisilobadilika la Mungu! Ni kila neno la maandiko "***lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu makosa yao, na kwa kuongoza, na kwa kuwaadhibisha katika haki"*** **2 Timotheo 3:16.**

Ni nani au ni nini kitapondapondwa?

Mataifa yatapondapondwa visehemu sehemu! kwa njia gani? Miundo ya mpingakristo na sheria ambazo zimewekewa watu ili zipinge injili kuhubiriwa; ambazo zinawaweka wachungaji korokoroni kwa kubandirisha watu; ambayo inasababisha vifo kwa wale wanabandirisha watu wawe wakristo na kadhalika. Ni miundo kama hii ya serekali na sheria ambazo zinapinga BWANA na Kristo wake ambazo zitapondapondwa **(Zaburi 2:1-12).**

Roho wa Eliya

Wengine wamesema kuwa roho wa Yezebeli haswa ni adui wa huduma ya kinabii na urejesho wa huduma ya kiunabii ya siku za hapa karibuni. Hata hivyo katika maandishi ya kitabu cha wafalme, Eliya anawakilisha zaidi ya huduma ya kiunabii. Kwa uhakika Eliya ni mfano wa Mfalme na Kuhani.

Katika taifa la Israeli katika wakati huo, **Eliya alikuwa na huduma ya kikuhani** kwa kuwa alikuwa ameruhusiwa kutoa sadaka **lakini pia alikuwa na huduma ya Kifalme** kwa kuwa mamlaka halisi katika taifa ilikuwa juu yake na mfalme Ahabu alitii neno la Bwana kupitia Eliya. Kisha katika **Ufunuo 2** Yezebeli anatakiwa kushindwa na kanisa katika Thiatira, sio ashindwe na nabii kama vile, lakini ashindwe na kanisa. Ni kanisa ambalo limevikwa roho wa Eliya ambalo linainuliwa katika nyakati hizi za mwisho kumshinda Yezebeli.

Ujuzi wetu katika urejesho wa kiutume ni ule wa kufuatilia na kuendelea kushambulia kutoka kwa roho ya Yezebeli. Roho ya yezebeli ni roho ya shetani ikijaribu kuzuia kanisa kutawala na kutamalaki hapa ulimwenguni, Kama vile Yezebeli aliangamizwa kabisa kwa neno la Bwana vivyo hivyo roho ya Yezebeli itashindwa na neno la Bwana.

Kampuni cha ushindi

"Na mtoto wake kushikwa juu hata Mungu, na kwa kiti chake cha enzi"* (Ufu 12:5).** Mtoto huyu ni **kundi lote** kama vile mwanamke anayejifungua ni kundi lote. Mtoto mwanamume [mtoto mume] inaweza kumaanisha 'wana wa Mungu'; inaweza kumaanisha kundi la kiutume; inaweza kumaanisha kikundi cha washindi. Hii yote ni njia ya kueleza mabaki ya kanisa ambalo inazaliwa na kuinuliwa nyakati hizi za mwisho. "Wakinyakuliwa hata kwa Mungu na kwa kiti chake cha enzi"*** haimaanishi kuondolewa [kunyakuliwa] kwa kanisa kutoka ulimwenguni, lakini inaonyesha asili ya uhusiano ambayo kikundi hiki kiteule [mtoto mwanamume] aliyo na Mungu: **Wanatembea na Mungu kwa njia ya kubadirishwa kama vile Henoko alitembea na Mungu, na ni mwili mtakatifu wa washindi ambao wanajua mamlaka ya Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme [enzi yake], ambao wanahubiri na kuuwakirisha ufalme wake hapa ulimwenguni.** Kikundi kama hicho kitatawala mataifa!

Tunanyakuliwa namna gani kwa Mungu na kwa enzi yake?

Ni kwa kuzaliwa kutoka mbinguni **(Yohana 3:3)**; Ni lazima tuzaliwe na Roho ili tuingie ufalme wa Mungu (**Yohana 3:6**). Tangu nizaliwe mara ya pili nilifahamu ya kuwa mimi ni sehemu ya Ufalme wa Mungu. Mungu ni Baba yangu na Bwana Yesu Kristo ni Mfalme. Kama kuna ufalme ni lazima kuwe na enzi.

Asiri ya kutembea kwa kikristo ni kuwa imewekwa tukomae kutoka watoto ndani ya Kristo mpaka tutawale na tutamalaki na Kristo katika ufalme wake. Kikundi cha wana wa Mungu ni lazima kizaliwe; kisha **panakuwa na muda wa kukua kabla ya wana wakomae na kutembea na Mungu kwa njia ambayo ufalme wake unadhihirika kupitia hao.**

Mwana wa Mungu mwenyewe alikuwa ndani ya tumbo ya mama yake kwa kipindi cha kawaida; kisha ni lazima angekua mpaka miaka 30. Kisha akahudumu kwa miaka mitatu na nusu, akidhihirisha ufalme wa Mungu, akikamilisha kazi ambayo Baba alikuwa amempatia aifanye. Tunaandaliwa sasa kwa wakati wa kudhihirishwa kwa **Kristo kwa ajabu ndani yetu,** matokeo yakiwa kwamba mataifa yote watakuwa na nidhamu kupitia neno la Mungu na hatimae Babeli itaanguka.

Vita mbiguni

Matokeo ya mtoto mwanamume kuzaliwa ilikuwa, ambaye sasa anatembea na Mungu kwa njia ya uhusiano wa ajabu, ni kwamba ***"Vita vikatokea mbinguni"* (Ufu 12:7).** Tambua ya kwamba vita mbinguni zilikuwa kati ya "***Mikaeli na malaika zake na yule joka na malaika zake."*** Vita mbinguni ni za BWANA! Kanisa halijaitwa kufanya vita mbinguni.

Kama matokeo ya vita, Shetani, "***Audanganyaye ulimwengu wote, akatupwa nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye"* aya 9.** Kanisa limeitwa lishinde katika ulimwengu! Vita vyetu ni dhidi ya mshtaki wa wandugu ambaye amerushwa kutoka mbinguni. Ushindi wetu uko katika msingi ya kwamba "***Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake umekuja"* aya 10.**

Kanisa linawazaa wana

Kutoka kwa kanisa la kweli ambalo limefanywa na waamini waliozaliwa mara ya pili, wana wanazaliwa ulimwengu kote. Ujumbe wakufanywa wana ulitangazwa makumi ya miaka hapo awali na waanzilishi wengine lakini sasa ni wakati wa kutimizwa kwa ujumbe huu. Kuna kuzaliwa kwa wana wa Mungu! Hawa wana katika kuwakilisha wanajulikana kama **mtoto mwanamume**, kama **kikundi cha washindi, mwili uliokomaa** wa waamini. Katika kikundi cha kiutume ni vyepesi kuwa na mbegu hii ya uwana ikizaliwa ndani yako. Kisha pana kipindi cha kukua na kuja katika ukomavu na kujifundisha kutembea katika ukomavu. Tunaweza kuwa sehemu ya kikundi hiki cha mtoto mwanamume! Tunaweza kuwa sehemu ya mwanaume mtoto kampuni!

Kanisa linawazaa wana.
Wana hawa watakuwa ni jeshi, kikundi cha watu wanaoshuhudia
ambao watakuwa hawasimamishwi, hawapotoshwi;
kikundi cha kiutume ambacho kitatawala mataifa kwa fimbo ya chuma.

ASILI YA WATU WANAOSHINDA

Ufahamu na utendaji wa watu wa kiutume

Bwana anafunua asiri ya kanisa lote kwa kuleta ufahamu na matendo ya watu wa kiutume. Katika siku za Nuhu saduku la wokovu lilikuwa ni mashua, lakini **katika siku hizi za mwisho saduku la wokovu ni kanisa la Yesu Kristo.** Hii inahitaji ufahamu kamili na wa ndani wa kanisa la kweli kama ilivyo funuliwa katika Agano Jipya.

Wale 120 katika chumba cha juu

Ufahamu wa kikundi cha kiutume unakuja kwanza kutoka kwa mfano wa wale wanafunzi 120 ikihusisha mitume na uongozi wao, ambao walidumu katika chumba cha juu katika kutii Yesu katika **mdo 1**. Hawa wandugu waliendelea katika dua na sala na walikuwa katika "***Shauli moja".*** Jukumu kubwa likipewa Petro na Roho Mtakatifu ilikuwa kuweka mtume mwingine ili msingi ambao kanisa litakapojengwa uwe umekamilika.

Kikundi ni cha kimaandiko

Baadaye katika kitabu cha **Matendo** tunapata kukitajwa *"**Wenzao"*** **(Mdo 4:23, 21:8)** na ***"vikundi"*** **(Mdo 15:22).** Picha ya kikundi kama ufahamu wa vile Agano Jipya linafanya katika ushirika wa kujipatiana inapatikana katika maandiko na ni wazo la Mungu. Kwa miaka kadhaa sasa tumekuwa tukitii kuendelesha tabia ya kikundi Shiloh kama vile Bwana ametuelekeza kufanya. Kikundi hiki hakihusishi tu watu wa palepale lakini wandugu wanahusiana katika kanisa la nyumbani na vikundi vidogo hata maelfu ya kilomita mbali.

Mamlaka na ulinzi katika kikundi

Wakati kikundi cha kiutume kinaanza kufanya kazi **kunakuwa na mamlaka makuu na ulinzi ambazo zinaachiliwa kwa sababu ya kazi ya huduma.** Mwezi wa Tisa/wa kumi mwaka wa 2007, kikundi kilitoka katika kikundi cha kiutume cha SHILOH kuhudumu Afrika ya Mashariki, London na USA. Katika maandalizi ya safari hii kulikuwa na maombi mengi ya kukubaliana katika kikundi yaliyofanyikia SHILOH. Ujuzi huu wa maombi ulikuwa na nguvu sana kwamba tuliona kilichokuwa kikitoka hakikutumwa kutoka kwa kikundi lakini [kama ilivyoonekana katika mkutano wa maombi ya pamoja] walienda pamoja ng'ambo kupitia kikundi ambacho kilikuwa kinatoka. Tulizungumzia jambo hilo kiunabii kabla ya kuondoka na kisha tukaona uhakika wake tulipokuwa ng'ambo.

Mmoja katika shughuli ya kiutume

Haikuwa tu kikundi kilichoondoka ambacho kilihisi ngazi hii mpya ya kuunganishwa katika kikundi cha kiutume na kuhisi utendaji wake hata katika taifa la mbali, bali hata wapendwa kule nyumbani hata katika nyuma zilizotengwa njuu na chini ya East coast ya Australia, pia walihisi ngazi mpya ya kuunganishwa na kuwa mmoja katika safari ya kiutume ambayo ilikuwa ikiongozwa na kikundi kilichokuwa kikihudumu ng'ambo. Kulikuwa na ushindi nyumbani na ng'ambo kwa sababu tunaanza kuwa **kikundi cha washindi.**

Kwa damu ya mwana kondoo

Ufunuo 12:11 Yatufundisha kuwa ushidi juu ya Shetani mstaki wa wandugu, inawezekana tu tukiwa pamoja kama mwili wote wa waamini, ukiungamanishwa pamoja. Maandiko yasema "***walimshinda***".Ni watakatifu wakiunganishwa pamoja katika kikundi cha kiutume – watu ambao

ni kielelezo – ambao wamejipatiana kutembea katika ukomavu, ambapo "***Damu ya mwana kondoo"*** inafanya kazi kuwapatia watakatifu ushindi.

Damu ya mwana kondoo yafanya kazi namna gani?

"*Bali tukienda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake yesu, mwana wake, yatusafisha dhambi yote"* (1Yohana 1:7). Wapendwa, ni ya muhimu kwamba tutembee pamoja katika nuru ya Yesu Kristo tukiongozwa na Roho wake katika nuru ya neno lake, tukiwa wazi, wenye ushirika wa kuheshimiana na kupendana na kujipatiana kwa mmoja na mwingine katika kumcha Kristo. Maisha ya kujipatiana kwa wapendwa katika kumuogopa Mungu ni ishara ya maisha yaliyo jaa Roho Mtakatifu **(Efe 5:18-21)**.

Kwa hivyo wakati wowote kunatokea uzito, kutokubaliana, kutoelewana ama shinda nyingine ikiinuka miongoni mwa wapendwa, nilazima kupunguza hesabu na tupatane kwa haraka kwa mmoja na mwingine katika kumcha Kristo. Hivi ndivyo ***"damu ya Yesu Kristo"*** inafanya kazi katika mwili: wakati wowote shinda (dhambi) inatokea, nilazima ishughulikiwe mara moja kwa toba na kukili, tukiruhusu damu ya Kristo kutakasa. Hivyo uhusiana katika mwili unarejeshwa kwa haraka, tukiruhusu ushirika wa kweli na kuwawezesha watakatifu kutembea katika nuru pamoja.

Ijapokuwa kuna umuhimu wa kila mtakatifu kutembea katika nuru ya Yesu Kristo, ni ujuzi wa kikundi chote na kujieleza ambayo Mungu anaangalia – kanisa linalotembea katika ukomavu – na ni kujieleza kwa pamoja ambako litamshinda mstaki wa wandugu, ikiwezesha washiriki wote katika ushirika kutembea katika ushindi.

Mwili ukifanya kazi pamoja

Wakolosai 3:12-17 ni kielekezo chenye nguvu cha kuishi pamoja katika mwili wa Yesu Kristo. Mungu anatarajia mwili kufanya kazi hivi, ***"Mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyo wasamehe ninyi, vivyo na ninyi."*** Tunaweza kupuuza haraka mafundisho wazi na mwelekeo wa Mungu kupitia maandiko ambayo anatuagiza jinsi tunapaswa kutembea na kujiendesha katika uhusiano katika mwili.

Kikundi cha kiutume kinatajwa kama '***wateule wa Mungu'*** na "**wateule"** wanapaswa "***kujivika moyo wa Rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu".*** Maneno haya yote ni ya uhusiano, ikielekeza nia zetu na matendo yetu katika uhusiano wa washirika wengine katika mwili. Kisha maandiko yanasema "***Jivikeni upendo…na amani ya Kristo iamue miongoni mwenu".*** Haya yote ni katika mazingira ya mwili.

Kwa neno la ushuhuda wao

Pili walimshinda mstaki wa wandugu "***Kwa neno la ushuhuda wao".*** Tambua tena ni kukili kwa pamoja, '***Ushuhuda wao'.*** Hii inatupeleka tena katika **Wafilipi 3:15-17** "***Basi sisi tulio wakamilifu na tuwaze hayo…natuenede katika lilo hilo".*** Natuwe "**Watu kielelezo"!**

Ungamo la kitume

Neno la ushuhuda wao ni ungamo la kitume ***"Imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** **Yuda 3.** Huu ndio ushuhuda: **ufahamu wa siri; ushirika wa siri (Efe 3:2-11).** Uhakika wa **kufanyika wana (Efe 1:5).** Ni kwa kikundi, kanisa lote, ambapo Mungu anapatiana ***"nia ya Kristo"*** (**1 Wakorintho 2:16).**

Moja wapo wa stakabadhi za kufanywa upya ni kukili kwa Westminister.Baba zetu wa imani katika nyakati hizo walifahamu umuhimu wa '**ungamo'.** Neno 'kukiri' kwa kiyunani

‘*homologeo’* yamaanisha ‘kuongea neno moja’. Inatumika kwa nguvu katika **Warumi 10:8** ambapo ‘**twakili wokovu wetu’**, tukiamini katika mioyo yetu.

Neno hili ‘ungamo’ ina jambo la ‘*tangazo la hadhara la kuungamanisha ambapo uhusiano wa kisheria unaimarishwa kwa muda’* (SFLB p.1566). Kumbuka twapaswa kuwa na kukili kwa Yesu mtume wetu **(Waeb 3:1).** Kukili kwa namna hiyo kumekosekana kanisani kwa miaka 1800. Imekuwa ni kukosekana kwa ushuhuda kwa **kanisa lenye asiri ya kiutume** ambayo imeelekeza kwa ukosefu wa ushindi katika historia ya kanisa hivi punde.

Sisi ni akina nani

Neno la ushuhuda wetu ni ufahamu wetu na kukili sisi ni akina nani: **mwili wa kristo, wateule wa Mungu, watakatifu**, na **wito wetu mkuu** [kufikia kufufuliwa kwa wafu, (**Wafilipi 3:11**)] katika **kusudi la Mungu** ambalo alilikamirisha katika Kristo Yesu (**Efe 3:11**) na sasa anatimiza katika kanisa siku hizi za mwisho.

Ushuhuda huu unahusisha ufahamu wa siri, ***“ushirika wa siri”*** **Efe 3:9,** ambapo Mungu anakusudia ***“hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho”*** **Efe 3:10.**
Unaweza kuona vile kanisa kwa pamoja linatembea katika ushindi, likimshinda mstaki wa wandugu?

Hawakupenda maisha yao hata kufa

Ya tatu walimshinda “***hawakupenda maisha yao hata kufa”.*** Huu ni utendaji kazi wa **1 Yohana 3:16** ***“katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu***”. Kutoyapenda maisha yetu hadi kufa inasungumsa habari ya kujipatiana kwetu katika ushirika, kwa kikundi cha kiutume na kufurahia kuwekwa pahali petu katika mwili wa Kristo “***mlinunuliwa kwa thamani”*** **(1 Wakorintho 7:23**)

Thamani ya mwisho ni kufia imani, na kufia imani sio tu ‘kufa kwa sababu ya imani’ lakini pia ni kuyatoa maisha yetu kwa sababu ya maisha ya rafiki zetu. Siku za hivi karibuni Bwana ameiweka wazi kwetu yakwamba anataka ‘**tutoe maisha yetu kwake na kwa mmoja na mwingine’.** Hii ndio asiri ya kikundi cha kiutume. Nimeyatoa maisha yangu kwa ndugu zangu. Ndugu zangu wameyatoa maisha yao. Kama uhakika wa ‘**kutoyapenda maisha yetu hadi kufa’** inajulikana kwetu, uhusiano wa kujipatiana ambao tunafurahia unafanyika ukuta wenye nguvu dhidi ya mashabulizi, ambayo mara nyingi yanakuja kupitia mastaka.

Tunapoanza kutembea katika ufunuo wa kikundi cha kiutume, wa ushirika wa kikristo na jamii, tutahisi kwa pamoja ushindi juu ya yule muovu na utukufu wa Kristo utathihirishwa zaidi na zaidi ndani na kupitia watakatifu.

KAMPUNI YA KITUME

Kikundi cha kwanza cha kiutume

Tunapo soma aya za kwanza za kitabu cha **Matendo** tunaona kuundwa kwa kikundi cha kwanza cha kiutume. Kikundi hiki kinahusisha mitume ambao walikuwa na Yesu, ***"Wanawake, na Miriamu mama yake Yesu, na ndugu zake"*** **Mdo1:14,** pamoja na waamini wengine, ***"Jumla ya majina ilikuwa mia na ishirini"*** **Mdo 1:15b.** Walikuapo waume na wake ambao walikuwa na umoja na kusudi moja (**Mdo 1:14 na 2:1**); walikuwa ***"moyo mmoja na roho moja"*** **Mdo 4:32.** Kikundi hiki cha kiutume kilikuwa kimejipatiana kwa maombi. Ni kupitia maombi ambapo Petro aliongozwa na Roho kumchagua Mathias ili achukue pahali pa Yudas kama mtume wa kumi na wawili.

Kikundi kiteule cha wanafunzi

Mfano wa kwanza wa kikundi cha kiutume ulikuwa ni wanafunzi wateule wenye nia moja, wakiendelea katika sara na dua; ni kwa kikundi hiki ambapo Mungu alimtuma Roho, akitimiza sikukuu ya pentekote na kuwaachilia mitume kuhudumu kuliinua kanisa la Bwana Yesu Kristo.

Wakiwa na uwezo wa kuwapokea waamini 3000

Petro alikuwa na uwezo wa kusimama kwa niaba ya wale kumi na mmoja na kuhubiri ujumbe wenye nguvu kuhusu Umasihi wa Kristo Yesu, akielekeza watu ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" Mdo 2:38.*** Kikundi hiki cha kiutume kiliandalika na kikawa tayari kupokea waamini 3000 kwa siku moja! Na pamoja ***"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate na katika kusali".*** **Mdo 2:42**

Roho wa kufanyika Wana

Mitume ambao Yesu alifundisha walikuwa wameandalika na tayari kupokea utimilifu wa Roho wa kufanyika wana na walikuwa na uwezo wa kufanya kazi kiwango kama cha Yesu. Ujuzi wa **Mdo 2** kwa kikundi cha kiutume katika chumba cha juu ilikuwa tofauti kwa ujuzi wa kuokolewa kwa waamini [3000] ambao walibatizwa siku hiyo na kupokea kalama ya Roho Mtakatifu. Ujuzi wa wale 120 ulikuwa tofauti katika kujazwa Roho ambapo watu wa mataifa walipokea katika nyumba ya Kolinelio **(Mdo 10)** ama ujazo mwingine [ubatizo] wa Roho Mtakatifu katika kitabu cha **Mdo.**

Ujuzi wa pentekote

Ufufuo wa Pentekote ambao ulianza kalne ya ishirini na imeendelea kwa sababu ulikuwa urejesho wa ujazo au ubatizo wa Roho Mtakatifu. Haukuwa urejesho wa utimilifu wa Roho ya Uwana. Roho wa kufanyika Wana unarejeshwa leo!

Ni wakati wa ukomavu, sio wakati wa Pentekote. Hatimaye Pentekote ni mojawapo wa misingi lakini kufanyika wana ni njia ambayo kanisa lililokomaa linafika kwa hatima yake, ambayo ni utukufu wa kristo ukifunuliwa watakatifu wake hapa ulimwenguni.

Kuitwa ili uwe mtu wa kiutume

- Kuitwa kutoka katika ulimwengu ili kumfuata Yesu,
- Kuyaacha yote ili kutafuta ufalme wa Mungu kwanza;

- Kuuchukua msalaba kujikana na kuyakumbatia mateso kwa sababu Yake,
- Kuondoka kushuhudia na kuhudumu kote ambapo Bwana atakutuma,

Kutii wito huu kunahitaji kujipanga upya kikamilifu kwa maisha ya mtu na kuyapa kipa umbele malengo ya maisha nakujihusisha katika utendaji ili kutoshea katika wito wa Mungu.

Wito wa Mungu sio kuwa Mkristo mzuri tu; sio maisha yaliofaulu katika jamii kama ndio mwisho; sio kufaulu katika juhudi za biashara, ila iwe tu ni mapenzi ya Mungu. Wito wa Mungu ni kutimiza kusudi la Mungu: "***Tumeitwa kulingana na kusudi lake".*** Kusudi la Mungu linajulikana kwetu kupitia ufahamu wa siri **(Efe 3:1-11)**

Mungu anainua vikundi vya kiutume

Tumeitwa kuwa sehemu ya kikundi cha kiutume: kuungamanishwa **'kwa shauri moja, 'moyo mmoja na roho moja'** Kama mwili wa waamini katika **Mdo 1-4.**

Katika siku hizi Bwana anainua vikundi vya kiutume, likiongozwa na mitume, pakiwa na huduma zote tano, ili kufanya kazi kama mwili. Kila sehemu ya mwili ***"Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga mwenyewe katika upendo"*** **Efe 4:16.**

Mungu anatazama kikundi cha kitume ambapo ataongeza nafsi 3000 kwa siku moja! Kwa njia nyingine unaunda vikundi leo ambao wanaweza kupokea Roho Mtakatifu katika utimilifu ili wawe mwili wa Kristo unaofanya kazi hapa ulimwenguni.

Vikundi vya kiutume ndio viongozi

Vikundi vya kiutume ndio viongozi ambao Mungu anainua katika siku hizi ili adhihirishe kwa watu wake ushindi ambao ametupa juu ya ibilisi shetani. Vikundi vya kiutume zinapoanza kufanya kazi katika utimilifu wa mamlaka ya Masihi hapa ulimwenguni, kisha umati wa waamini watakapokusanyika na kukumbatia utume na kanisa hatimaye litafika kwa hatima yake: Kutawala na kutamalaki na Yesu aliye Masihi katika Sayuni. Katika siku za urejesho ambazo tumetunikiwa kuishi, Mungu ameamua kufanywa kwa vikundi vya kiutume kote ulimwenguni.

Kikundi cha kiutume ni:

- Mwili wa watakatifu ambao wameitwa pamoja katika kujipatiana
- Kuona kwamba ufalme wa Mungu umaeimarishwa ulimwenguni miongoni mwa mataifa.
- Watakatifu hawa wameitwa kutoka kwa idara na mashirika katika kutembea kwa utiifu ulio wazi kwa Kristo na neno la Mungu.
- Katika makundi hayo huduma zote na kalama ambazo Mungu amepatia kanisa katika Agano Jipya zinapata nafasi yake na kujieleza kikamilifu.
- Makundi haya yametanda katika mataifa; yanaongozwa na mitume;
- Yanafuatwa na washiriki wote wa makundi wakiwa na ufahamu wazi wa wito wa Mungu na ufunuo wenye nguvu wa kufanyika wana.

Vikundi vya kiutume ndio kielelezo cha kanisa

Kati ya mwaka wa 2001 Bwana alituagiza kuunda kikundi cha kiutume na kati ya miaka ametuangazia na ufahamu na utendaji kazi wa vikundi vya kiutume. Kikundi cha kiutume kinainuliwa na Bwana kuwa watu ***"kielelezo".***

Paulo anatazama haya kutoka **Wafilipi 3:15-17** ambapo ananena juu ya wale "***waliokamilika***" kwamba ***"Wawaze hayo"*** na "***kufuata mfano tuliowapa".*** Mapema katika **1Wakorintho 2:6-16**, Paulo anataja ***"Hekima ya Mungu katika siri"*** ambayo ni ya wale waliokomaa kupokea na hekima hii "***Mungu alipanga kabla ya wakati kwa sababu ya utukufu wetu".***

Mungu amekusudia kanisa lije katika ukomavu na ni ya muhimu kanisa kuja katika ukomavu kuweza kupokea ufunuo wa siri na kuanza kufurahia na kutembea katika utukufu wa Bwana.

Katika siku hizi za mwisho wazo la **'kanisa'** imekuwa ya kutatanisha sana wengi wakiona jengo au dini au idara kama kanisa. Kwa hivyo Mungu haswa anainua vikundi vya kiutume ili wawe muundo wa Agano Jipya.

Tambua Paulo anasema ***"Tunayo nia ya Kristo"*** **(1 Wakorintho 2:16)!** Ni kwa uhakika ya wingi! Hakuna mshiriki mmoja wa mwili atakaye kuwa na '***nia ya Kristo"*** peke yao lakini ni uhakika wa pamoja. Ni kikundi (Mwili wote) ambapo kanisa litashinda Shetani na kudhihirisha ushindi wa Kristo kati ya watu wake.

Kuitwa ili tuwe kanisa la kiutume

Kanisa la kiutume la Agano Jipya haikuwa dini ama idara na haitakuwa hivyo kwa kanisa la mwisho la kiutume. Kila pahali karibu nasi waamini na viongozi wa kikristo wanakubaliana, hakika bila kufahamu wito wa Mungu wazi kama ilivyowekwa na Yesu na Mitume katika Biblia au tu kupuuza yale ambayo Biblia inanena wazi. Wakristo kama hao wanapendelea jia na tamaduni za watu kuliko kutii neno la Mungu, wasitofautishe kutii dini au tamaduni za watu kuliko kuaminika katika kutii neno la Mungu. Mitume wa kwanza walipata changa moto kutoka kwa viongozi wa dini siku zao na wakaambiwa ***"msifundishe kwa jina hili. Petro na mitume wakajibu, wakisema, 'imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu'"*** **Mdo 5:28-29.** Vivyo hivyo Yesu anatazamia kanisa leo limtii Mungu kuliko wanadamu.

Yesu asatahili kuadhimishwa

Mara mingi mtu anapo shuhudia imani yake ndani ya Yesu, swali linalotokea ni hili, huwa unaenda kanisa gani?' Mawazo ya mtu na tabia za kanisa kihistoria zimeinuliwa kuliko Yesu, ila hali Yesu anastahili siku zote kuwa ndiye aliyeinuliwa juu ya mambo yote **(Wakolosai 1:18).** Wakristo mara nyingi wanaongea kuhusu makanisa yao na kinachoendelea katika makanisa yao [taratibu] kuliko kumhusu Yesu na kinacho tendeka katika kutembea kwao na Mungu. Hii ni kwa sababu tumeimiliki kanisa 'yetu' badala ya kuwa kanisa la Yesu Kristo kulingana na Agano Jipya.

Kuyafikia mataifa kupitia neema na utume

Katika **Warumi 1:5,** Paulo anatuambia yeye na kanisa la nyakati zake, mwili wa Kristo, ***"Tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani kwa ajili ya jina lake".*** Biblia inasema ni kupitia neema na utume zilizopokelewa kutoka kwa Baba kupitia Kristo ambayo inaelekeza kwa kujitiisha kwa imani katika mataifa.

Yesu alifundisha na kuchagua mitume kumi na wawili: Kwa hao aliwaaminia kuzaliwa na kuundwa kwa kanisa; kwa hao alipatiana funguo za ufalme wa mbinguni. Siku hizi za mwisho Yesu mara tena anawainua mitume ili walete msingi sawa wa kanisa lake na kuziita huduma zote na kalama ambazo zimepatianwa kwa sababu ya kulijenga kanisa. Kanisa ambalo Yesu anajenga leo litastahimili milango ya kusimu.

Kutoka Pentekote mpaka Mabanda

Nikupitia kikundi hicho cha kwanza cha kiutume ambapo Mungu alileta kutimizwa kwa sikukuu ya Pentekote na ni kupitia vikundi za kiutume ambazo Mungu anainua siku hizi za mwisho ambapo ataleta kutimizwa kwa sikukuu ya mabanda. Hili ni kanisa ambalo linaingia katika utimilifu wa yale yote Mungu ametenda ndani ya Kristo, ***"Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa mungu, kwa jinsi ya kimwili"*** **(Wakolosai 2:9*).*** Ni makusudi ya Mungu kuwa utimilifu wa Mungu udumu katika mwili wa Kristo. Hii ni sikukuu ya mabanda ikitimizwa: Mungu anakaa ndani ya watu wake; utimilifu wa Kristo ukifunuliwa katika kanisa lake.

"Yohana aliona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu" akasikia "***Sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema 'maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu. Naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye atakuwa Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao"*** **Ufu 21:2-3.** Hii ni kutimizwa kwa mambo yote! Huku ni kutimizwa ambao kutakuja baada ya Mungu kumtuma Kristo kutoka mbinguni (**Mdo 3:20**); huku ni kutimizwa ambako kunakuja baada ***"Hata zije zamani za kufanwa upya vitu vyote, zilizo nenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu"*** **Mdo 3:21.**

Kuangalia na kufunikwa kwa kikundi cha kiutume

Asiri ya watu wa kiutume ni kama ifuatavyo: Mungu ameinua vikundi za kiutume, amerejesha huduma ya mitume na kukusanyika pamoja katika uongozi wa huduma ya kiutume na watakatifu ambao wanafanyika kuwa roho moja na moyo kutumikia kusudi la Bwana siku hizi.
Bwana anakusanya vikundi ambavyo vinakuwa vya mitume wengine, manabii, wainjilisti, wachungaji na walimu, wasaidizi, viongozi, watakatifu wenye kalama, wanafunzi na waamini wapya katika kikundi.

Kila kiongozi muhuduma pamoja na muchungaji wanawajibika mmoja na mwingine katika uongozi wa wazee ambao wamejitiisha kwa neno la Mungu, wakitambua kwamba kila mmoja wetu anahitaji ***"mafundisho, kuwaonya, kuwaongoza, kuwaadibisha katika haki"*** **(2 Tim 3:16).** Wahuduma viongozi ambao Mungu amepatiana, haswa, mitume, manabii, na walimu **(1 Wakorintho 12:28)** lakini mara nyingi ikihusisha wachungaji, wainjilisti ambao wanahudumu kama wazee, wakitoa uongozi kulingana na uchaguzi wa Roho Mtakatifu (**Mdo 20:28)**

Yesu ndiye kichwa

Yesu Kristo pekee ndiye kichwa cha kanisa, ***"Naye ndiye kichwa cha mwili"*** **(Wakolosai 1:18) na anapatiana kivuli chote** cha upako wake kupitia Roho na mamlaka ya neno lake. Kanisa linatakikana ***"Kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo, Katika yeye mwili wote unaungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** **Efe 4:15-16.**

Mwili wote unahusiana na kichwa, Kristo. Hapana mtu aliyewekwa rasmi kuwa kiongozi wa kanisa katika maandiko. Kila muamini ni mshiriki wa mwili Wake na Kristo ndiye kichwa cha kila mshiriki na kila sehemu ya kanisa lake. Kwa hivyo kufunika hakitokani na mtu lakini kinakuja moja kwa moja kutoka kwa Bwana wakati kanisa limewekwa katika mpangilio wa kiutume.
AMEN!